Kikao cha Nne – Tarehe 18 Oktoba, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 75

Jeshi la Polisi Kujenga Nyumba za Kisasa Zanzibar

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza**:-**

Tunapenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwajengea askari wake nyumba za kisasa katika eneo la Kurasini (Kilwa Road) Dar es Salaam, kwa lengo la kuinua maisha ya askari hao na kuwawezesha kutekeleza majukumu ya ipasavyo.

(a) Kwa kuwa idara hiyo ni ya Muungano, je, kuna mipango gani iliyoandaliwa ya kujengwa nyumba kama hizo hapa Zanzibar.

(b) Je, serikali haioni kwamba askari polisi wanaishi katika nyumba duni za serikali ambazo majengo yake ni ya zamani na yashapoteza hadhi ya jeshi hilo.

(c) Mbali na jukumu la serikali kujenga nyumba za kisasa hapa Zanzibar, je, serikali inatekeleza vipi jukumu la kuzikarabati nyumba za zamani zinazotumiwa na askari polisi hapa Zanzibar katika maeneo mbali mbali, ikiwemo Ziwani Unguja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Baraza lako tukufu.

Aidha, namba nikushukuru wewe na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa ustahamilivu wao juu yangu. Baada ya shukrani hizo, kwa ruhusa yako na kabla ya kumjibu Mhe.

Mjumbe swali lake nambari 75 lenye vifungu (a), (b) na (c) namba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za kisasa kwa ajili ya nyumba za polisi ni utekelezaji wa mkakati wa programu wa maboresho yanayoendelea ndani ya Jeshi la Polisi. Lengo ni kuhakikisha kuwa askari polisi wanaishi katika nyumba bora na kuwajengea mazingira ya kuinua tija katika utendaji wao wa kazi. Kwa vile jeshi la polisi ni taasisi ya Muungano, ujenzi huo wa nyumba za kisasa kwa ajili ya makaazi ya askari unafanyika kwa pande zote mbili za Muungano wetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake lenvye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoeleza katika maelezo yetu ya msingi, mipango ya kuendeleza ujenzi wa nyumba hizo za kisasa za makaazi ya askari polisi kwa sehemu zote mbili za Muungano wetu ipo na inaendelea kutekelezwa kwa awamu.

Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kupitia mfuko wa taifa wa hifadhi ya jamii NSSF imo katika hatua za kuimarisha majengo mbali mbali kwa ajili ya makaazi na ofisi kwa matumizi ya jeshi la polisi. Kupitia mpango huu serikali imeweza kujenga majengo hapa Zanzibar.

Nyumba za makaazi huko Limbani Wete Pemba, nyumba za makaazi hapo Ziwani Unguja, Ofisi ya Jeshi la Polisi ya Mkoa wa Kusini Pemba, Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Chake Chake Pemba, Hanga ya Askari huko Ufikiwa Chake Chake Pemba, Hanga ya Askari hapo Bububu Wilaya ya Magharibi.

Aidha, hatua mbali mbali zilizochukuliwa kuhakikisha kwamba askari wetu wanapata mahala bora pa kuishi na kufanyia kazi.

(b) Mhe. Naibu Spika, serikali inatambua kuwa baadhi ya askari polisi wanaishi katika nyumba duni na haipendezi hali hiyo iendelee. Ndio maana serikali ikabuni mkakati wa kujenga nyumba za kisasa kwa ajili ya makaazi ya askari polisi.

(c) Mhe. Naibu Spika, serikali ina wajibu wa kukarabati nyumba zote mbovu zinazotumiwa na askari polisi. Ukarabati wa nyumba hizo unahitaji fedha nyingi na utaendelea kufanyika kutokana na jinsi uwezo wa fedha utakavyoruhusu, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Pamoja na majibu yake mazuri ya swali lililoulizwa, lakini alikiri kwamba kuna programu maalum na inatekelezwa sehemu zote mbili za Muungano. Mhe. Naibu Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri kwamba;

(a) Je,Mhe. Waziri, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina ushawishi gani kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kuharakisha ujenzi wa majenzi haya ili askari waweze kupata manufaa kwa wakati.
(b) Kwa kuwa askari polisi wanatumika katika shughuli mbali mbali za kitaifa nchini Zanzibar na ambao wametawanywa na wanashughulikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Je, kuna utaratibu gani wa mawasiliano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu utaratibu wa kuwaelekeza kazi askari hawa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba;

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar siku zote iko karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa kwa yale mambo yanayohusu mambo ya Muungano. Kwa msingi huu nachukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha kwamba miradi mbali mbali ya Jamhuri ya Muungano inayofanyika Zanzibar inatekelezwa ipasavyo. Kuna mahusiano ya Wizara zinazoshirikiana katika kukaa vikao mbali mbali vya kutafuta utatuzi wa matatizo ambayo yanajitokeza. Kwa hivyo, ushawishi mkubwa kupitia wizara husika vinapokaa katika vikao vyao kuhakikisha kwamba miradi inayoanzishwa Zanzibar inatekelezwa kama ambavyo imepangwa.

(b) Kuhusu utaratibu wa mawasiliano ni kama nilivyoeleza katika jibu langu la (a) kwamba kuna vikao vya pamoja vinavyokaa kati ya wizara husika ili kuzungumzia mambo mbali mbali ya utekelezaji mipango ya serikali hasa kwa yale mambo yanayohusu mambo ya Muungano.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuamka katika hali ya usalama na afya njema. Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

(a) Je, amezitembelea mara ngapi nyumba za maaskari kwa upande wa Zanzibar.

(b) Kama bado je, Mhe. Waziri anajua kwamba Wilaya ya Wete na baadhi ya sehemu za nyumba za maaskari, hasa Wilaya ya Wete ambako kuna sehemu tunaita *line*, kwamba kuna nyumba ambazo kwa kweli hata kukalika hazikaliki.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Asha Bakar anajua kwamba niliwahi kuwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, hivyo moja katika wajibu wangu ulikuwa ni kutembelea nyumba mbali mbali za askari polisi na vituo vya polisi. Nafikiri kazi hiyo niliifanya kwa umakini mkubwa.

Aidha, nataka nimuhakikishie Mhe. Asha Bakar kwamba ni kweli serikali inatambua nyumba za askari ziko katika hali mbaya na ndio maana kukaanzishwa mpango maalum

wa uboresho wa jeshi la polisi, msingi wake mkubwa ni kuimarisha makaazi ya askari, kujenga taaluma kwa askari wetu, kuhakikisha wanakuwa na vifaa vya kisasa na kupata mafunzo mazuri pamoja na maslahi yao kwa ajili ya kazi zao za kila siku. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe naomba nimuhakikishie kwamba serikali kadiri ya uwezo utakavyowezekana wa kifedha hatua zitachukuliwa ili askari wetu hawa wakae katika maeneo mazuri. Inasikitisha sana hali ile, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, angalau umeniona kwa mara ya mwisho kabisa, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa umekiri kwamba kwa muda mrefu kuna baadhi ya askari wanaishi katika mazingira duni. Je, serikali haihisi kuwaacha kwa muda mrefu kutaongeza kero za Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema katika majibu yaliyotangulia kwamba askari wetu huishi katika nyumba ambazo hazina hadhi stahili, sio vizuri hata kidogo na haipendezi. Ni nia ya serikali ya kufanya maboresho ili askari wetu hawa waweze kukaa katika hali nzuri.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba tatizo hili halipo upande mmoja tu wa Muungano, lipo kwa pande zote mbili za Muungano wetu, ipo Zanzibar na ipo kwa upande wa Tanzania Bara. Mimi nimepata bahati ya kutembelea kambi mbali mbali za polisi huko Tanzania Bara hali ni kama hiyo na wakati mwengine hapa Zanzibar kuna unafuu ukilinganisha na wenzetu upande wa Bara. Lakini jitihada zitaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba jeshi letu la polisi wanapata makaazi mazuri na mashirikiano yanaendelea. Hili ni tatizo ambalo linahusiana zaidi na mambo ya kifedha na mara hali ya kifedha itakapokuwa nzuri basi askari wetu hawa watapata makaazi mazuri.

Nam. 32

Uingizwaji wa Fedha kwa Wizara kila Robo Mwaka

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Pamoja na serikali kuandaa na Baraza la Wawakilishi kupitisha bajeti ya mwaka 2011/2012, kumekuwa na kasi ndogo sana ya uingizaji wa fedha katika wizara takriban zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa vifungu mbali mbali vya kasma vilivyopitishwa, hali inayoelezewa kukwamisha utekelezaji wa kazi nyingi za wizara zinazohusika kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

(a) Ni sababu zipi zimepelekea Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutoingiza fedha hizo kwa wakati na kwa kima kilichoamuliwa katika miezi mitatu iliyopita.

(b) Wizara inawaeleza nini wananchi wanaotegemea huduma muhimu za jamii ambazo kupatikana kwake kutafikiwa tu iwapo wizara zinazotoa huduma hizo

zitaingiziwa fedhe zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa wakati na kwa kima kilichopitishwa.

(c) Ni lini wizara itaacha mwendo huu wa kukwamisha utekelezaji wa wizara nyengine kwa kucheleweshe kuingiza fedha zilizoidhinishwa na kutoa kwa kiwango kilichopitishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa kabla sijajibu swali la Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya Baraza lako tukufu kupitisha bajeti ya serikali kwa mujibu wa matakwa ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, hatua inayofuatia ni utekelezaji wa bajeti hiyo, ili iweze kutekeleza mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimaye serikali iweze kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kupitia wizara mbali mbali, kwa kutumia vifungu vya kasma vilivyopitishwa na Baraza lako tukufu. Utekelezaji wa matumizi ya serikali huwa unategemea sana hali halisi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na upatikanaji wa mapato yanayotokana na wahisani.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa katika robo ya kwanza kiujumla hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ilikuwa nzuri, kwani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kukusanya jumla ya bilioni 48.6, sawa na asilimia 90 ya lengo na shilingi bilioni 53.4.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa misaada ya kibajeti mpaka kumalizika kwa robo ya kwanza, washirika wa maendeleo walikuwa bado hawajatoa fedha walizoahidi. Hali hii imepelekea kurudisha nyuma utekelezaji wa mipango ya serikali. Kwa mujibu wa mipango ya fedha za serikali, fedha za washirika wa maendeleo kwa kiwango kikubwa zimepangwa kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida katika robo ya kwanza, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia jumla ya Shs. bilioni 49.6 sawa na asilimia 99.5 ya lengo la Shs. bilioni 49.8.

Mhe. Naibu Spika, matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo hayakuwa ya kuridhisha kutokana na kuchelewa kuingizwa kwa fedha za misaada ya kibajeti, hivyo kupelekea serikali kutumia mapato yake ya ndani, angalau kulipa yale matumizi ambayo hayawezi kusubiri. Jumla ya Shs. bilioni 3.6 zilitumika. Maombi ya fedha za miradi kutoka mawizara mbali mbali kwa robo ya kwanza yalikuwa ni bilioni 12.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mhe. Ismail Jussa Ladhu, lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miezi mitatu ya awali ya bajeti, serikali imeziingizia wizara Shs. bilioni 49.6 kati ya bilioni 49.8 sawa na asilimia 99.5

kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shs. bilioni 3.6 kati ya Shs. bilioni 12, sawa na asilimia 30 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Sababu za msingi za kutokufikia lengo ni kuchelewa kupatikana kwa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

(b) Mhe. Naibu Spika, napenda kuwahakikishia wananchi kuwa serikali itakuwa karibu sana na wananchi katika kuwapatia maendeleo. Hata hivyo, ni vizuri tukaelewa kuwa serikali inaendeshwa na kodi kwa maana hiyo wananchi tuna wajibu wa kulipa kodi ili tuweze kupunguza utegemezi kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Vile vile nawaomba wananchi kujituma zaidi na wafanyabiashara kujikita zaidi katika kuwekeza vitega uchumi vyao ndani ya nchi kwa lengo la kuwapatia wananchi ajira na hatimaye serikali kupata mapato.

(c) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali kuwa matumizi ya serikali yanategemea upatikanaji wa mapato. Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo haicheleweshi utoaji wa fedha, bali wakati mwengine kunakuwa na upungufu wa mapato, hivyo hulazimika kutoa fedha chache iliyopo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pia namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kina, lakini pamoja na majibu hayo naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu waziri kakiri mwenyewe kwamba kumekuwa na matatizo ya upatikanaji wa fedha za washirika wa maendeleo, lakini hili linaeleweka kwa sababu katika ripoti za serikali siku zote katika Baraza hili, mara nyingi upatikanaji wa fedha za washirika wa maendeleo zimekuwa hazipatikani kama inavyotarajiwa. Kwa hivyo, kupanga bajeti kwa kutegemea fedha hizi kupita kiasi katika kipindi cha mwanzo inaonekana kwamba haukuwa mpango mzuri.

Swali langu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba

(a) Je, hizi fedha ambazo anasema ameziingiza, je atakubaliana na mimi kwamba zimeingizwa katika mwezi wa Septemba tu hivi karibuni na ndio maana yake zikasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi kutokana na kuzikosa katika miezi ya Julai na August.

(b) Mhe. Naibu Spika, suala la uingizwaji wa fedha linaonekana linasimamiwa na Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, lakini anayeiandaa bajeti ni Afisi ya Bajeti katika wizara hii. Kwa nini utaratibu usibadilishwe kwamba anayeamua kiwango cha kupelekwa katika wizara mbali mbali na afisi yake isiwe ni idara ya bajeti na Afisi ya Mhasibu Mkuu ikabakishiwa jukumu la kulipa tu, baada ya kwishabajeti kuelekeza ambayo ndio inayopanga bajeti hiyo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba safari hii tumezungumza na wafadhili tukiwa pale Marekani kwenye mkutano wa Benki ya Dunia na mawaziri wa fedha kutoka katika nchi mbali mbali. Tanzania tumeeleza *concern* yetu kwa wafadhili, tumewaelezea kwamba kiutaratibu *discussion* inakamilika mwezi wa Mei, ndio maana tuna- *approve* ile bajeti yao na tunaipeleka kwenye bajeti zetu Bungeni na Barazani kwenye mwezi wa Juni. Au *expectation* ni kwamba Julai fedha hiyo itaingia na kuweza kufanyakazi. Wanapochelewa kututilia hizo fedha, maana yake tunachelewesha maendeleo ya wananchi wetu na sisi tunakuwa hatuna majibu ya moja kwa moja kwa wananchi wetu.

Kwa hivyo, tumewaomba sana kwamba tuheshimu mijadala yetu na tuheshimu makubaliano yetu. Pia wao wameliona hili na tunaamini kwamba sasa litaanza kutekelezwa kwa sababu tulikuwa tuko *very serious* katika hili, sisi Zanzibar pamoja na wenzetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini la msingi ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu amesema ni kwamba fedha zimeingia mwezi wa Septemba. Ni kweli. Ukitazama katika *background* yetu yote ukenda katika takwimu za miaka yote utagundua kwamba mara nyingi mwezi wa Julai na mwezi wa August mapato ya serikali yanakuwa kidogo yana upungufu. Hii ni kutokana na kwamba wafanyabiashara huwa wanaisubiri bajeti, wasikilize kuna kodi gani zinazopandishwa. Mara nyingi huwa mwezi wa Juni huwa hawaleti vitu vikaingia mwezi wa Julai, vinavyoingia vinakuwa ni vichache sana, mpaka wapate ile *confidence* ya bajeti huwa ndio wanaanza kuagizia vitu vya kuanzia mwezi wa Julai, halafu vinakuja kutiririka mwezi wa August na Septemba.

Lakini kimsingi ni kwamba huwa tunatakiwa sisi Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tuwape ile *quarter* yao kwa ukamilifu hata kama tumewapa mwezi wa Septemba, wao wenyewe wanaelewa wizara jinsi ya kuweza kupanga matumizi yao kwa mujibu wa fedha ambazo tumewatilia. Kwa hivyo, hili ni *trend* ya kawaida, ukitizama takwimu zetu mapato utaona mwezi Julai na August yanakuwa kidogo yana upungufu. Lakini kiutaratibu inakuwa pale ambapo mapato yanapopatikana mwezi wa Septemba tunatakiwa tukamilishe na ndio maana takwimu zinatuonesha kwamba tumetoa asilimia 99.5.

Suala la pili, ni kweli alivyosema Mhe. Ismail Jussa kwamba muandaaji wa bajeti ni kamishna wa bajeti na msimamizi na mtoaji wa fedha ni mhasibu mkuu. Lakini nataka nikuambie tu sasa hivi mhasibu mkuu yeye ni mtoaji tu. Tuna kamati ya makatibu wakuu, tunaita, *the ceiling committee* inakutana kila mwezi, inaangalia mapato yetu na inapitia mahitaji ya wizara moja baada ya moja, halafu wanaangalia mapato yetu na umuhimu wa kila kilichoombwa. Ndio pale anaambiwa mhasibu mkuu sasa wewe toa kwa mujibu wa makubaliano. Kwa hivyo, hata kama ukimuondoshea mamlaka haya ambayo anayo kisheria na kikatiba mhasibu mkuu, bado kamishna wa bajeti itabidi atizame hili hili ambalo analitizama muhasibu mkuu. Utoaji wa fedha unategemeana na mapato na vile vile inategemeana na *ceiling committee* walipogawa zile fedha kwa mujibu wa mahitaji, kuna mambo mengine hayawezi kusubiri na mengine yanaweza kustahamili.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali kama ifuatavyo. Kwa kuwa utekelezaji wa bajeti ya serikali kunatokana na upatikanaji wa fedha zilizokadiriwa kupatikana katika kipindi kile na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa pamoja zimekubaliana kuwa fedha za *income tax* zinazokatwa kwa wafanyakazi wa Muungano wanaofanyia kazi Zanzibar zilipwe katika hazina ya Zanzibar. Swali langu liko hapa.

(a) Je, Mhe. Waziri utekelezaji wa suala hilo ukoje mpaka sasa.
(b) Ni kiasi gani cha fedha kinategemewa kupatikana kutokana na fedha hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kamati inayosimamia kero za Muungano tumekubaliana kwamba fedha za *income tax* kwa ajili ya wafanyakazi wa Muungano wanaofanyakazi Zanzibar zilipwe Zanzibar.

(a) Nathubutu kusema kwamba fedha hizo hazijaanza kulipwa bado kutokana na sheria ile haijafanyiwa marekebisho, inategemea kupelekwa kufanyiwa marekebisho katika Bunge lijalo kwa mujibu wa maelezo tuliyoyapokea kutoka hazina Tanzania Bara.
Mara tu wakishakuifanyia marekebisho ile sheria basi zile fedha zitaanza kulipwa moja kwa moja Zanzibar.

(b) Tunatarajia kupata bilioni 18 katika kipindi cha mwaka huu kwa wastani wa bilioni 1.5 kwa kila mwezi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja lenye vifungu viwili kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kitendo kilichotokea cha kuingizwa kwa fedha hizi, ni udhibitisho wa hasa wa kutegemea fedha za wafadhili katika miradi yetu ya maendeleo, ambapo tunawategemea kwa zaidi ya asilimia 90 katika fedha za kuendesha miradi yetu ya maendeleo.

(a) Je, katika funzo hili tulilolipata la kutokuzipata fedha hizo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka, serikali inachukua hatua gani za dharura za kuimarisha mapata yetu ya ndani sambamba na kubuni vianzo vipya vya mapato ili kuondokana na aibu hiyo tegemezi.

(b) Kwa kuwa kuna kila dalili zinazoonyesha kwamba fedha hizi huwenda tukazipata katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka. Je, zitakapopatikana serikali italipa *area* katika kipindi cha robo ya kwanza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nikubaliane naye kwamba kuna haja kubwa, ninawaomba sana

Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane sana katika hili kutafuta mapato zaidi, ili tupunguze utegemezi. Katika hili nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba mambo ambayo tunayachukua pale wizarani, la kwanza ni kuyaangalia mapato tunayokusanywa na wizara yale ambayo ni makubwa, sasa kuyahamishia ZRB yaani yakusanywe na ZRB.

Lakini jambo la pili, tunataka tuwahamasishe wafanyabiashara wa ndani kuwekeza ndani, ili tuweze kupata mapato zaidi na ajira zaidi hapa ndani.

La tatu, tunataka na hili tuko katika mazungumzo na tunategemea kuyakamilisha na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika, ili kuwasaidia wananchi wetu wale wafanyabiashara wadogo wadogo, waweze kukua zaidi na hatimaye wataendelea kulipa kodi zaidi.

Jambo la nne, tunataka tuifufuwe kwa haraka zaidi sekta ya uvuvi, ili iweze kusaidia katika kupata mapato zaidi. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi ni shahidi, tunahangaika sana na katika kipindi cha hivi karibuni uvuvi utakuwa ni moja katika tegemeo letu hapa Zanzibar.

La tano, nyinyi wenyewe ni mashahidi mulipokuwa mkichangia jana, mulijaribu sana kumuelekeza Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwamba sio karafuu tu aangalie na viungo vyengine, hiliki na pilipili manga zote hizo tunataka tu tuwahamasishe wakulima wetu walime, ili ziweze kutuletea mapato zaidi.

Mhe. Naibu Spika, swali lake la pili kama nilivyoeleza fedha ambazo tumezipanga za wahisani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kweli fedha hizi zitakapoingia basi tutawapa miradi ile tuliyoipangia asilimia 100 kwa mujibu wa fedha zitakavyoingia. Kwa hivyo, fedha zao watapata, ili waweze ku-*speed* utekelezaji wa miradi yao ya maendeleo na wala hatuna ujanja zitakavyoingia basi ndivyo tutakavyoweza kuwapa. *(Makofi)*

Nam. 53

Rushwa kwenye Mahakama

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Suala la rushwa kwenye mahakama zetu limekuwa tatizo kubwa katika nchi yetu na ambalo linakwaza utoaji wa haki.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako imechukua hatua gani kulikomesha tatizo hilo, ili wananchi wapatiwe haki zao bila ya vikwazo?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 53 kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na ukweli kuwa yapo madai mengi yanayoihusisha Taasisi ya Mahakama na upokeaji wa rushwa. Madai haya yapo pia kwa takriban vyombo vyote au vingi vya utendani na utoaji wa haki. Kwa kweli ni suala ambalo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hailitaki hata kidogo na itaendelea kulikemea kwa nguvu zake zote.

Mhe. Naibu Spika, rushwa inatokana na vishawishi vingi kama vile mazingira ya kufanyiakazi pamoja na nafsi yake mtu mwenyewe. Kwa upande wa mazingira ya kutendeakazi kama vile maslahi mazuri, vipando, nyumba za kuishi ni changamoto kubwa.

Kwa upande wa maslahi ya wafanyakazi hao wa Mahakama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeshaanza kuchukua hatua angalau za kuwaongezea maslahi yao, pia tutaendelea kujitahidi pale tutakapopata uwezo wa kuwasaidia katika maeneo mengine ya usafiri na makaazi.

Mhe. Naibu Spika, nafsi ya mtu nayo ni sehemu moja ya kichochozi cha rushwa, hivyo lazima kila mtu ailinde nafsi yake. Kwa upande wa serikali katika kuhakikisha kuwa haki ya mtu hainunuliwi au haikataliwi kwa sababu mhusika hakutoa rushwa, basi serikali imeshaandaa Mswada wa Sheria ya Rushwa ambao utaletwa katika Baraza lako tukufu katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachofuata kwa ajili ya kujadiliwa. *(Makofi)*

Naamini sheria hii nayo itasaidia sana katika kupunguza au kuondoa kabisa suala la rushwa na wala si kwa Mahakama tu bali hata maeneo mengine ya utoaji haki. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi wakati itakapoletwa sheria hiyo, basi tuijadilini kwa kina pamoja na kuipitisha, ili ianze kazi mara moja.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine na kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunawaomba watendaji wote wa serikali kujiepusha na tabia hii mbaya ya kuchukua rushwa kwa huduma ambazo ni wajibu wake mtendaji huyo kuzitoa. Kwa hivyo, yeyote atayekiuka miko hii, basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mhe. Manajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri ni kesi ngapi za rushwa ambazo ziko Mahakamani kwa hivi sasa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, swali hilo siwezi kumjibu ni kesi ngapi zilizoko Mahakamani hivi sasa, kwa sababu sina takwimu hizo kwa muda huu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, utamjibu kwa maandishi?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naweza kumjibu kwa maandishi ikiwa atataka na baada ya kulifanyiakazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri. Hivi serikali ingependa Wawakilishi pamoja na wananchi kwa jumla watafsiri vipi hatua za serikali hii za kutotekeleza ahadi zake katika Baraza hili kuhusiana na suala la rushwa.

Kwa mfano, katika kikao kilichopita serikali iliahidi kuleta katika Baraza hili kwenye kikao hiki kinachoendelea Ripoti kuhusu Kadhia za Baraza la Manispaa pamoja na Ununuaji wa Mitambo ya TVZ kwa jina la mtu binafsi na tuliahidiwa katika kikao hiki lakini haikuletwa.

Je, vitendo hivi vya serikali havileti tafsiri kwa Wawakilishi pamoja na wananchi kwamba serikali haiko makini na badala yake imekuwa ikitoa ahadi za maneno kuliko vitendo zaidi? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, nafikiri Mhe. Mjumbe anajua kwamba kuna masuala ya kisheria yanayoitwa *separation of powers* na pia kuna masuala ya kisheria ambayo yanataka kutokuingiliana kwa kufanyakazi katika wizara moja na nyengine.

Kwa hivyo, suala la Manispaa linahusiana na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wao walisema kwamba wataleta, lakini unapopeleka taarifa katika chombo kama hiki Mhe. Naibu Spika, basi ni lazima taarifa ile iwe imekamilika na wala haina utata, pengine katika tume hiyo kazi imeshamalizika.

Sasa inapomalizika na kupelekewa kiongozi anayehusika, basi anawajibika kuirejesha tena kwa kufanyiwa kazi, ili taarifa zilizopungua ziweze kujazwa. Kutokana na hali hiyo, mimi siwezi kumjibia waziri anayehusika, lakini naamini suala hilo baada ya kukamilika basi litaletwa Barazani kama ilivyoahidiwa.

Nam. 39

Uhaba wa Vyuo vya Ufundi

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Wizara itakubaliana na mimi kwamba kuna uhaba wa Vyuo Vikuu vinavyotoa taaluma ya ufundi ukilinganishwa na Tanzania Bara, jambo hilo ni kikwazo cha maendeleo ya watoto wetu ambao sasa wamekuwa na hamu ya kusoma fani mbali mbali.

Serikali ina mpango gani wa kuongeza Vyuo Vikuu vitakavyofundisha masomo ya ufundi katika viwango vya *degree* na kuendelea?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe, swali lake Nam. 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa nchi yetu ina uhaba wa Vyuo Vikuu vinavyotoa taaluma ya ufundi ukilinganisha na Vyuo Vikuu vilivyoko Tanzania Bara. Hadi hivi sasa hakuna Chuo Kikuu kilichopo Zanzibar kinachotoa mafunzo ya shahada ya fani ya ufundi.

Hata hivyo, ninafuraha kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba mipango ya kutoa mafunzo ya shahada ya fani mbali mbali za ufundi katika Vyuo vyetu Vikuu inaandaliwa.

Chuo Kikuu cha *SUZA* kinatayarisha kuanzisha Kitivo cha Uhandisi katika Kampasi mpya ya Chuo Kikuu huko Tunguu. Kitivo hiki kitaanza na kutoa mafunzo ya shahada ya ufundi wa *computer*. Vile vile Chuo Kikuu cha Zanzibar (*Zanzibar University*) kilichopo Tunguu kimeanza kazi za ujenzi wa Kitivo cha Uhandisi. Aidha Taasisi ya Sayansi ya Karume inatarajia kutoa mafunzo ya shahada ya ufundi ifikapo mwaka 2013. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Nashukuru kupata fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina mkakati gani wa kuhakikisha tunakuwa na vyuo mbali mbali vitakavyotoa *course* tofauti kama vile *International Relationship and Good Governance* na kadhalika?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza katika swali letu mama kuwa mipango ya serikali ndio hii ambayo nimeshaieleza mbele ya Baraza lako tukufu. Lakini kwa yale ambayo bado hatujajitayarisha nayo, basi tunashirikiana na vyuo vya wenzetu vilivyoko Bara wanafunzi wetu kuchukua taaluma hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwanza napenda kuipongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuona haja ya kuendeleza elimu ya ufundi na kutupatia bango zuri la Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Naomba kumuuliza Mhe. Waziri tokea lilipobandika lile bango, yaani tulipopitisha sheria hii kuna mabadiliko gani ya chuo kile yaliyofanywa na wizara, ili kuhakikisha kwamba tunaelekea huko? *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, mafanikio yapo na hata kama akipitia bajeti yetu ambayo tuliipitisha mwaka huu hapa Barazani kwenye ukurasa wa 54 mpaka 55 kuna maelezo ya mafanikio ambayo yamefikiwa na Chuo chetu cha Karume. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa amekiri wizara ikishirikiana na vyuo iko mbioni kutekeleza masomo ya mafunzo ya fani za ufundi. Vile vile kwa kuwa wananchi wameshazoea kusikia serikali iko mbioni. Hivi unaweza kuliambia Baraza hili tukufu ni lini hasa mafunzo haya yataanza hapa Zanzibar? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali langu mama kwamba nilieleza hatua mbali mbali ambazo tayari zimeanzishwa na vyuo vyetu. Pia nilieleza kuwa Chuo chetu cha Karume kinatarajia kuanzisha shahada ya mafunzo ya ufundi ifikapo mwaka 2013. *(Makofi)*

Nam. 8

Uuzwaji wa Bidhaa Zilizomaliza Muda wa Matumizi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Serikali imeanzisha Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, ili kuyalinda na kuyanusuru maisha ya wananchi. Hata hivyo, pamoja na kuanzishwa kwake bado kuna tatizo kubwa la kuingizwa na kuuzwa kwa vyakula, madawa na vipodozi ambavyo vimemaliza muda wake wa matumizi na vyengine havina kiwango.

(a) Je, Mhe. Waziri anafahamu kwamba maisha ya wananchi yako hatarini kutokana na matatizo ya matumizi ya bidhaa hizo?

(b) Wizara ina mpango gani wa kushirikiana na taasisi nyengine kama vile Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Baraza la Manispaa, ili kukabiliana na tatizo hilo?

(c) Ni bidhaa za aina gani na kiwango gani ambazo zimekamatwa na bodi hiyo kuanzia Julai 2010 hadi Juni 2011, ambazo zilikuwa sokoni wakati hazifai kwa matumizi ya binadamu?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 8 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafahamu athari zinazopatikana na matumizi ya vyakula, dawa na vipodozi vilivyomaliza muda wake na vilivyochini ya viwango. Ndio maana mnamo mwaka 2006 Baraza lako hili tukufu lilipitisha Sheria Nam. 2 mwaka 2006 na kuanza kutumika Januari mwaka 2007, ili kukabiliana na tatizo hilo.

(b) Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ina wajumbe kutoka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Baraza la Manispaa pamoja na Serikali za Mitaa, hivyo wanashirikiana kwa karibu katika ukaguzi, uchunguzi pamoja na uangamizaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

(c) Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Juni 2011 bodi ilikamata na kuteketeza bidhaa ambazo zilikuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu kama ifuatavyo:-

- Tani 24.4 za mtama;
- Tani moja ya mchele aina ya Basmat;
- Asali ndoo sita zenye ujazo wa lita 120;
- Chumvi kilo mbili;
- Zabibu;

- Tende tani 2;
- Maziwa ya watoto makopo 24 aina ya NAN na Lactogen 1, pamoja na makopo 20 ya maziwa aina ya NAN 1.
- Dawa za aina mbali mbali tani 3 na
- Boski 37 za mafuta ya kupikia aina ya *Super Sun Oil*.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizojiimarisha sana katika mambo ya ulinzi na usalama kwa kuwa na vikosi vingi vikiwemo vile vya SMT na SMZ. Vile vile ni juzi tu tulipitisha ile Sheria ya Viwango katika Baraza hili.

(a) Je, Mhe. Naibu Spika, inakuwaje bidhaa hizi zilizokosa viwango zikawafika watumiaji bila ya kuchukuliwa hatua au kuzuiliwa?

(b) Kwa kuwa kuna mambo kama haya ya *chemicals* ambazo huwa zinatumika hususan kwa wanawake katika masuala ya kujibadilisha. Kwa mfano, *Jik* au hizi *bicarbonates* kwa ajili ya kujichubua. Je, ni lini wizara yake hizi dawa ambazo sio kazi yake katika masuala ya kijipamba itatoa semina kwa akinamama kwa lengo la kuwapa maelekezo hasa kwamba matumizi ya dawa hizi si kujipamba, isipokuwa ni *chemicals*?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika,

(a) Suala la kwamba vipi vyakula hivi vinafika walaji ni suala ambalo inawezekana vilipoingia vilikuwa bado vizima na uchunguzi unafanywa pale bandarini. Lakini baada ya kukaa muda kwenye maghala ndipo vinapogundulikana kuwa vimepitwa na wakati na hii ni moja katika tabia ambayo ni mbaya. Kwa mfano, chakula kinaweza kuingia nchini kumbe vile kina muda wa miezi mitatu au sita ku-*expire*.

Wakati mwengine inawezekana uwekaji wake kwenye ghala kwamba mwanzo kilikuwa kizuri, lakini ghala iliyowekwa ikawa ina unyevu ama hawakufuata taratibu na ndipo huharibika.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana bodi yetu mbali ya kuvikagua au kuvitizama wakati vinapoingia pale bandarini, basi pia huwa wanapita kwenye maghala kwa ajili ya kukagua pamoja na wale wenye kuuza, ili kuona hali halisi ya mambo. Mhe. Naibu Spika, baadhi ya hivi vitu ambavyo tumevieleza vilikutikana ghalani na kupigwa marufuku visitumike zaidi.

Kwa hivyo, inawezekana vikapiga bandarini kizima na baada ya miezi sita hakijamaliza kuuzwa kikakutikana si kizuri.

(b) Kuhusu akinamama, nakumbuka jana ulikuwa mjadala na ulitoka kwako hapa Mhe. Mjumbe kuhusu mambo ya uhai na nilijibu kwamba kuna pia haki ya mtu kuchagua anachokitaka. Kwa kweli tutajitahidi kuwaita akinamama na kuwaeleze kwamba ni hatari kwa nyuso pamoja na miili yao. *(Makofi)*

Lakini masuala ya kujipambamba pamoja na urembo haya ni mambo ya hiari. Kwa mfano, leo nimevaa suti tofauti na ya jana na wala hakuna aliyeniambia ni uamuzi wangu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mtandao wa Biashara ya Vyakula, Madawa na kadhalika umeenea nchi nzima, kwa sababu wananchi ndio wanaotumia. Kwa bahati mbaya vijijini au mashamba vifaa kama hivi ambavyo pengine zimesha-*expire* kwa muda mrefu sana na kule hakuna utaratibu watu kupita na kuchunguza vitu hivi na watu wanaendelea kutumia tu.

Je, ni siku gani wizara husika itajipanga kikamilifu hasa na kazi hii iliyofanywa mijini mpaka kupatikana chumvi kilo mbili ambazo zimesha-*expire* itaenea vijiji vyote, ili walaji tuweze kulindwa? *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba huduma za aina ya kitaalamu zinazofanyika mjini haziko nyingi mashamba. Lakini naomba nimueleze Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwamba kuna mashirikiano makubwa sana kwa Vikosi vya Ulinzi pamoja na viongozi mbali mbali kama vile Masheha na Viongozi wa Wilaya.

Kwa kweli hivi sasa Mtandao wa kufuatilia Madawa ya Kulevya umeimarika sana na hivi juzi Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar Hoteli ya Bwawani ametuambia kuna Ulinzi Shirikishi, ambao umeweza kumaliza baadhi ya sehemu kukosekana hata yale madawa ya kulevya.

Sasa siku gani tutafika vijijini ni suala la kuimarisha huduma zetu mpaka vijijini. Kwa hivyo, hilo naahidi kwamba tutalifanya kila tutakapopata nafasi ya kuongeza watendaji wetu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, je Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba vipodozi hivyo hawatumii wanawake tu peke yao mpaka wanaume? *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kukubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba hata wanaume wanatumia. Lakini swali niliulizwa linahusu wanawake ndio nilijibu kwa wanawake. *(Makofi)*

Nam. 65

Ajira kwa Vijana

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Katika juhudi za kukuza uchumi wa nchi za Asia pamoja na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wa nchi hizo, serikali za nchi hizo huibua miradi mikubwa ya maendeleo inayowaajiri watu wengi.

(a) Je, Serikali ya Zanzibar ina mpango gani kuiga mifano mizuri ya nchi hizo?

(b) Kwa kuwa vijana wengi sasa hawana kazi, serikali imeandaa utaratibu wa kuwapatia ajira.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto) – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 65 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kimsingi wizara haioni tatizo lolote la kujifunza mifano mizuri itakayosaidia kuwapunguzia tatizo la ajira vijana wetu, iwe mifano hiyo Afrika, Asia Ulaya au hata sehemu nyengine yoyote ya dunia.

Serikali imeunda Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, ili kusimamia kwa karibu zaidi tatizo la ajira kwa vijana wetu wa Zanzibar.

(b) Mhe. Naibu Spika, kutokana na Mfumo Huru wa Uchumi na Ubinafsishaji, Sekta Binafsi inatarajiwa kuchukua nafasi kubwa zaidi ya kutoa ajira kwa vijana. Hivyo, serikali inaandaa mazingira ya kuona vijana wake wanao uwezo wa kuingia katika Soko la Ajira kwa kuweka mipango pamoja na sera zinazotoa fursa kwa vijana ndani na nje ya nchi.

Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu (a) kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika nao kwa upande wao wanayo mipango mizuri tena mingi ya kutoa ajira kwa vijana wetu, ili kuwapunguzia ukali wa maisha haya.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Hivyo, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba hivi sasa katika Sekta za Binafsi hususan sehemu za hotelini wengi ni watu ambao kutoka Kenya na Wazanzibari hawana nafasi ya kupata kazi.

Je, wizara yako ina mpango gani wa kulikamilisha suala hili, ili Wazanzibari waweze kupata ajira hizi tulizokusudia serikali kuwawekea na kukuza uchumi?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba katika mahoteli wafanyakazi wengi vijana hawa ni kutoka nje ya Zanzibar lakini kuna sababu.

Moja ya sababu hizo ni kwamba vijana wetu wa Zanzibar hawataki kujielimisha katika masuala haya. Pili ni kuwa vijana wetu wa Zanzibar kuna kazi nyengine hawazipendi kama vile za kutandika vitanda, kukata majani na kadhalika. Sasa ikiwa wao hawazitaki na muajiri anataka kufanyiwa shughuli zake, basi lazima aajiri kutoka pahala pengine.

Kwa mnasaba huo mimi napenda kutoa wito kwa vijana wetu kwamba nafasi katika mahoteli zipo, isipokuwa wajitahidi kusoma, kujiendeleza katika sekta hii na wala wasichague kazi, kwa sababu kazi ni muhimu kwao wao. Kwa hivyo, wakifanya hivyo tunaweza hatua kwa hatua kuwaondoa hawa wageni na vijana wetu wa Kizanzibari wakapata nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ajira inategemea na taaluma na elimu yetu zaidi ni ya nadharia. Je, serikali ina mpango gani wa kutanua Elimu ya Amali ya kweli kweli ya Uvuvi ufundi na mengineyo ili kuwapa nafasi vijana kuajiriwa katika sekta ya binafsi hasa ya viwanda na kwengineko.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto) Ni kweli kwamba katika sekta hizi ambazo zinahitaji elimu hasa hizi elimu ambazo ni za utendaji wa kazi hasa elimu za amali, kuna haja kwa sisi binafsi kujiendeleza katika masuala hayo na serikali imeona matatizo hayo na umuhimu wa kuwa na elimu kama hiyo, ndio maana serikali ikahakikisha kwamba inaanzisha vyuo vya amali katika maeneo au katika Mawilaya yetu yote na pili ikaunda Wizara ya Kazi Ajira na Uwezeshaji Kiuchumi ili wao kuweka mikakati mizuri na mikakati bora zaidi ya kuwasaidia vijana wetu katika shughuli hizi.

Kwa hivyo naamini Wizara ya Kazi, Ajira, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wao hivi sasa wameshaandaa mipango mizuri ya kuwasaidia vijana wetu katika shughuli hizi za ajira aina kama hii ambayo umesema.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri kama alivyosema kwamba vijana wetu hawapendi baadhi ya kazi kama vile kukata majani na kutandika kitanda mchanga, lakini kwa kuwa chuo cha utalii cha Maruhubi kinatoa taaluma sana katika masuala haya ya utalii, kwa kuwa si kweli kwamba vijana wetu hawapendi kazi za kutandika vitanda na kukata majani wanapenda hata za kuosha vyoo. Lakini inaonekana kwamba wawekezaji katika sekta hii ya utalii ni wabaguzi wanapenda sana kuajiri wageni kulikoni wazawa.

a) Je, ni lini serikali itawapa masharti ya uwekezaji kwamba lazima kwanza waajiri wenyeji halafu ndio watafute wageni.

b) Kwa kuwa akina mama wengi katika ukanda wa Mashariki kule kwetu Pemba mpaka huku Unguja wamewekeza maisha yao katika masuala mazima ya kilimo cha mwani, na kwa kuwa suala zima la kupata mikopo benki na hata katika ile mikopo ya AK na JK inakuwa tabu sana na masharti mazito.

Je, ni lini serikali itawasaidia hawa kinamama ili waweze kujikwamua na kuongeza kipato chao kupitia mikopo hii?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto) : Kwa kuna nina hakika kwamba vijana hawa huwa hawapendi kazi hizi kama nilivyosema mwanzo na kwa kuwa Mhe. Mwakilishi amesema kwamba mahoteli haya yana ubaguzi, basi mimi Wizara yangu ya Wanawake na Watoto tukishirikiana na na Wizara ya Kazi, Ajira, Uwezeshaji Kiuchumi tutalichunguza suala hili kwa makini tutizame, kama hivyo ndivyo basi namhakikishia kwamba hatua nzuri muafaka itachukuliwa ili kuwasaidia vijana wetu hawa.
Lakini zaidi ningelisema niseme kwamba kwa sababu sisi tuna uhakika kwamba baadhi ya kazi hizi vijana wetu hawazipendi, basi na hayo yote tujaribu kuwashawishi ili kuwaelimisha zaidi kwamba na wao waweze kuchukua nafasi hizi kwa maslahi yao na maslahi ya Wazanzibari.

Lakini pili suala la kuwawezesha wanawake mimi nafikiri suala hili lilizungumzwa katika maeneo mengi, moja ni suala lile ambalo kuna mitaji ya JK na AK ambayo inawasaidia wanawake na watu wengine katika kuwaendeleza katika shughuli zao za kiuchumi, lakini pia nakumbuka kwamba lilizungumzwa suala la kuwa na benki ambayo inaweza kusaidia mambo haya. Suala hili la benki naamini bado linafanyiwa kazi na hapo litakapofikia hatua nzuri na muafaka na ikiwa tutaweza kumudu utaratibu au masharti yale ambayo yanatakiwa kuanzisha benki aina hizi basi naamini hatua hizi zitachukuliwa ili tuzidi kuwaendeleza wanawake pamoja na watu wengine katika kujiendeleza kimaslahi na kiuchumi.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri napenda niongeze kidogo tu ni kweli kama alivyoeleza kwamba vijana wetu kumekuwa na hii tabia ya kuchagua kazi, lakini na ukweli upo kwamba waajiri hawawapi nafasi Wazanzibari *(Makofi).*

Katika hilo napenda niwahakikishie wajumbe kwamba Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na Ushirika, imeanza kuchukua juhudi ya kuwaita waajiri wote wa mahoteli tumezungumza nao na kutokana na zoezi hili la kuwaita tumefanikiwa katika kipindi cha Julai hadi Septemba vijana kama kumi na tano (15) wamepata ajira kutokana na utaratibu huo tulioutumia kwa hivyo tutaendelea.

Lakini vile vile kuna tatizo wanapolalamika Mameneja wa Mahoteli wanasema kwamba vijana wa Kizanzibari wanashindwa hata kufanya zile *interview*, sasa hivi tumeandaa utaratibu maalum wa mafunzo ya kuwapa *training* namna ya kukabiliana na hili tatizo, tunatarajia katika kipindi cha miezi mitatu basi vijana wetu kadhaa watapata ajira katika maeneo hayo pamoja na hayo pengine ni kutandika vitanda na mengineyo. Ahsante sana.

Nam. 51

Mitambo ya TVZ iliyodondoka Baharini

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza:

Tunaipongeza Serikali kwa kuwa na nia ya kuwezesha wananchi wa Pemba kuiona Televisheni Zanzibar. Kwa bahati mbaya mitambo iliyokusudiwa kutimiza azma hiyo ilidondoka baharini wakati wa kushushwa kwenye Meli ya Serengeti. Kwa kuwa serikali ina azma ya kudai fidia kwa wamiliki wa meli hiyo.

a) Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha kilichotwza Meli hiyo ikiwa ni fidia baada ya vyombo hivyo muhimu kuharibika.

b) Fedaha hizo zinatarajiwa kulipwa ndani ya muda gani.

c) Endapo mdaiwa atashindwa kulipa fedha hizo ndani ya muda uliowekwa hatua gani zitachukuliwa dhidi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, mitambo siyo iliyodondoka baharini, zilizodondoka ni betri za UPS, idadi yake ni nane (8) vile vile ifahamike wazi kuwa tatizo lilitokea wakati wa kuteremsha mzigo, tatizo sio la mwenye meli kama ilivyoelezwa kenye barua hiyo, tatizo ni la shirika la Bandari.

a) Gharama zote hizo wastani ni randi 40,504.97 sawa na shilingi 9,316,143.10 za Tanzania

b) Muda mfupi tunatarajia kutatua tatizo hilo.

c) Barua ya madai ya fidia imeshapelekwa kwa Mkurugenzi Mku wa Shirika la Banadri na tunasubiri majibu ya barua hiyo ya madai. Hata hivyo hakuna tatizo la fedha hizo wenzetu wameonesha nia nzuri tu na wametoa mashirikiano mazuri sana na wanaonesha nia ya kulipa.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Muda mfupi ni mwingi je Muda mfupi ni muda gani huu uliokusudiwa kulipwa vifaa hivyo.

b) Je, Mhe. Waziri alipokwenda kufuatilia vifaa hivyo walikwenda kama Wizara.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Makubaliano haya hatukuweka muda lakini wana nia safi ya kulipa pale mahitaji yatakapokamilika.

Mhe. Mwakilishi kwa kweli Wizara yangu kwa kushirikiana na Afisa Mdhamini Pemba tulikwenda na tukaona ile hali iliyotokea ajali na tulifuatilia vizuri ndio maana kwenye suali mama nikaeleza hivi na nimefafanua vizuri Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.
Kwa kuwa mara nyingi malipo ya fidia huchelewa baina ya Wizara na Wizara. Je, makubaliano yenu yapo katika mkataba maalum kwa maandishi?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Ukweli hakuna mkaataba maalum lakini wenzetu wameonesha nia nzuri na tumekaa na tumezungumza hakuna hofu yoyote, nakuomba Mheshimiwa utoe hofu masuali yetu haya kama nilivyoeleza kwenye suali mama watalipa na tutashirikiana na mambo yetu yatakwenda vizuri kwa ujumla.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye sehemu a, b na c.

Kwa kuwa Mhe. Waziri Katika kikao cha bajeti aliahidi mbele ya baraza hili na wananchi kwamba mwezi wa Septemba matangazo yatapatikana, kwa kuwa hilo halikutokea.

a) Je, Serikali ilitoa taarifa kwa wananchi kueleza sababu zilizotokea matangazo haya yasipatikane sambamba na kuwaomba radhi.

b) Kwa kuwa suala la matangazo halikuonekana kama lilivyoahidiwa. Je sasa ni lini wananchi wa kisiwa cha Pemba watarajie kupata matangazo hayo.

c) Kwa kuwa Mhe. Waziri aliahidi na hakutokea wala hakuomba radhi. Je. Kwa nini asiitumie fursa hii kuliomba radhi baraza pamoja na kuwaomba wananchi radhi.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Ni kweli kwamba tulitoa ahadi hapa lakini tukasema kwamba haya ni masuala ya kiufundi lolote linaweza likaja kutokezea na ndio maana sikutoa tarehe kwa makusudi, kama mlivyosikia kulikuwa na vyombo fulani vilianguka na sisi hatukutarajia jambo lile.

Lakini pamoja na kwamba vimeingia kwenye bahari sio kwamba tunasubiri tufidiwe huku, sisi baada ya kufikia vile tumemwambia *agent* na hivyo vitu viko njiani vinakuja wakati wowote, hatusubiri kufidiwa na Shirika la Bandari. Shirika la Bandari itatufidia pesa sio vifaa na vilivyopotea ni UPS pamoja na batri.

Mitambo imeshafungwa na tumejaribu na inaonyesha lakini hatutaki kurizki, kwa sababu bila ya vifaa hivi tukifunga itaonyesha lakini UPS hiki ni chombo kinachohifadhi umeme pale umeme unapokatika ili matangazo yaendelee kwa hivyo hatutaki kuonyesha hivi sasa mpaka tuvipate hivyo vifaa, lakini naahdi na nina imani kwamba ndani ya mwezi huu basi vyombo hivyo vitakuwa viko tayari.

Kwa lile jengine labda niliahidi lazima nikubali kwa hivyo ninaomba radhi. *(Makofi)*

Nam. 42

Tatizo la Maji

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:

Mara nyingi hutokea uharibifu au matatizo katika Vituo vyetu mbali mbali vya maji na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji. Kwa kawaida kupita kitambo kabla ya Mafundi kutoka Mamlaka ya Maji (ZAWA) kufika katika vituo hivyo ili kuyaptaia ufumbuzi matatizo yaliyopo.

a) Je. Wizara haioni kuwa kuna umuhimu wa kuweka Mafundi maalum wenye ujuzi angalau mmoja katika kila Wilaya ili awe anatembelea, kukagua na kutengeneza sehemu zinazoharibika mara tu tatizo linapotokea.

b) Kuna sababu gani za msingi zinazopelekea Mafundi kutoka Mamlaka ya maji kuchelewa kufika vituoni kutatua matatizo yanayotokea huku wananchi wakishumbuka kufuata maji katika sehemu za mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Swali lake Nam. 42 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imeweka maafisa wa maji kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Mkoa kwa dhana nzima ya kutembelea kukagua, kutengeneza na kusimamia kazi za maji katika maeneo hayo ya kazi. Maafisa hao wanao uwezo wa kutosha kufanya kazi zao kiufundi na endapo ikijitokeza hitilafu yoyote ambayo iko nje ya uwezo wa kiufundi taarifa hizo hupelekwa Afisi Kuu kwa kupatiwa msaada wa vifaa na kiufundi.

b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu (a) mafundi wa Mamlaka hufika katika eneo la tukio mara tu wanapopata ripoti, na mafundi hao wanapofika hulishughulikia tatizo hilo na linapokuwa nje ya uwezo wao hurejea ofisini kwa kupata msaada wa kiufundi na vifaa.

Mhe. Mahamod Mohammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Pamoja na majibu yasiyo ridhisha ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyatoa ningelipenda tu kumfahamisha Mhe. Waziri kwamba katika eneo la Jimbo la Kikwajuni, maeneo ya Kilimani Jumba namba nane (8) kuna

tatizo la maji kupotea sasa hivi kiasi ya mwezi mmoja na Nusu mpaka miwili, tumefika kwenye Ofisi yako tumetoa taarifa na hakuna hatua yoyote ambayo imechukuliwa.

Je, Mhe. Waziri utatwambia nini katika hili wakati watu wana matatizo ya maji na maji yale yanapotea bila ya kwenda kuchukuliwa hatua zinazofaa katika kudhibiti upotevu ule wa maji yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Kwanza nakubaliana nae kwamba kuna tatizo kubwa katika jimbo la Kikwajuni hususan katika hili suala la maji, namuahidi Mheshimiwa Muwakilishi kwamba tunalishughulikia tatizo hilo na tutazidi kulishughulikia mpaka tufikie hatua iliyokusudiwa. Namuomba avute subra zaidi tunajitahidi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri atakubaliana nami kuwa hao maofisa aliowataja kutoka Wilaya na Mkoa kuwa hawafanyi kazi kutokana na vitendea kazi hawana. Hivi sasa hawana gari hata moja ya kuelekea maeneo ya shamba.

b) Kwa vile Mheshimiwa aliyeuliza suala hili la msingi anatokea jimbo la Muyuni na huko kuna kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Muyuni ikiwemo Pete, Muungoni na Kitogani. Je, tutegemee mwaka gani wananchi hao watafaidika na suala la maji.

c) Kuwachangisha wananchi maji wakati huduma hiyo haipo si kuwaonea wananchi hao. Je, kuna mpango gani wa kusitisha zoezi hilo la kuwachangisha wananchi mpaka itakaposimama huduma hiyo ya maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Sikubaliani na Mhe. Muwakilishi kwamba maafisa wangu hawafanyi kazi, vile vile sikubaliani kwamba hatuna magari lakini tuna upungufu wa magari lakini magari tunayo na ndiyo wanayotumia maafisa wangu kwa kufuatilia matatizo yao.

Namuomba Mhe. Muwakilishi astahamili kidogo tunajitahidi sio jimbo la Muyuni tu lakini hata jimbo la Nungwi lina matatizo sana ya maji, lakini wananchi wangu wanastahamili kwa vile wanajua serikali imejitahidi kulivalia njuga na tunamuahidi kwamba haya tukijaaliwa yatakaa sawa.

Kuhusu suala la kuchangia maji suala hili huchangia wananchi muda ule maji yanapopatikana lakini yakiwa hayapatikani basi wananchi hawachangii maji hayo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la msingi la Mheshimiwa ambalo aliuliza suala la kuharibika haribika mashine katika vituo vya maji na kupelekea matatizo makubwa kwa wananchi wetu.

a) Je, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri haoni hii kuharibika haribika mashine kwa maji kwamba Wizara yake inanunua mashine ambazo ziko chini ya kiwango.

b) Kama wananunua mashine ambazo ziko chini ya kiwango hatuoni kwamba tunaitia hasara serikali na vile vile kuwapa matatizo mengi wananchi ya kupata maji katika maeneo ya kwao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Wizara yangu hainunui mashine ambazo hazina kiwango, isipokuwa tu nataka ajue kwamba uharibikaji wa mashine unatokana na na hitilafu za mara nyingi zinazosababishwa na umeme ambao tunautumia hapa Zanzibar kwa kipindi hiki, lakini si kwa kununuliwa mashine ambazo hazina kiwango.

Nam. 18

Serikali Kulilinda Zao la Karafuu

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:

Ingawa Serikali imepandisha bei zao la karafuu, kuna taarifa kwamba baadhi ya wananchi walikuwa wanaziuza nje ya nchi kwa njia ya magendo.

Je, Serikali imejipanga katika kulinda zao hilo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: **-** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli kwamba zao la karafuu limekuwa tegemeo kubwa kwa wananchi wa Kisiwa cha Pemba na pia nakubali ni muhimu.

Ni kweli serikali imepandisha bei ya zao la karafuu ili kuhakikisha ina baresha maisha ya wakulima wa zao hilo na wananchi kwa jumla na pia kulirejesha zao la karafuu katika hadhi yake iliyokuwa nayo hapo awali. Aidha ni nia ya serikali kuhakikisha zao hili haliuzwi kimagendo, ingawa nikubaliane na Mhe. Kuwa kuna baadyi ya wananchi wanaziuza karafuu nje ya nchi kwa njia ya magendo.

Mhe. Naibu Spika, Serikali kupitia Wiara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na utafiti na mchakato wa kutayarisha mkakati ujulikanao kama *IP Value Capture Strategy* ambao utapelekea kupatikana kwa alama maalum *(Branding)* kwa zao letu la karafuu za Zanzibar, alama hii itafanya karafuu ya Zanzibar kutambulika katika ulimwengu wa kibiashara na itakuwa ni vigumu kwa mtu yoyote kuziuza kimagendo kama inavyofanyika hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe tusitoke kwa sababu tukishamaliza masuala tunategemea kumwita Waziri na kuweza kumaliza mswada wetu, kwa hivyo anayetoka arejee haraka ndani ili tumalize kazi tuliyokuwa nayo.

Nam. 94

Udhalilishaji wa Wananchi Wanaofanya Kazi Mahotelini

Mhe. Mohammed Said Mohammed **-** Aliuliza:

Wafanyakazi wengi wa Mahoteli hukosa haki zao za msingi kutoka kwa waajiri wao katika maeneo yao ya kazi na zaidi baada ya kufukuzwa kazi, hali ambayo pamoja na sababu nyengine huwafanya wafanyakazi hao kuhama hoteli moja hadi nyengine.

a) Kwa kuwa vitendo hivi vimeshamiri kwa muda mrefu, Je Wizara imechukua hatua gani kukomesha tabia hii mbaya ya kuwanyanyasa wananchi.

b) Je, kwa namna gani Wizarainajiepusha na dhana ya kuwapendelea wageni dhidi ya wananchi wetu wanyonge katika utatuzi na kuishughulikia migogoroya namna hii.

c) Je, ni malalamiko mangapi yanayohusiana na madai hayo yameshghulikiwa na Wizara kuanzia Januari hadi Septemba 2011 na mangapi yamepata ufmbuzi kwa maslahi ya wananchi wetu wanaodhalilika hotelini huko.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Swali lake Nam. 94 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Kwa kawaida Wizara kupitia Kamisheni ya kazi huwa inafanya ukaguzi kazi ikiwa miongoni mwa shughuli zake za kawaida. Madhumuni ya ukaguzi huo ni kuona kwa kiasi gani waajiri na waajiriwa wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria. Pale inapobainika kwamba kuna unyanyasaji katika sehemu ya kazi, basi maelekezo hutolewa ya kurekebisha hali hiyo na iwapo muajiri au muajiriwa ataendeleza tabia hiyo, basi hatua za kinidhamu huchukuliwa. Baadhi ya hatua ambazo zimechukuliwa na Wizara katika kuzuwia unyanyasaji katika sekta ya utalii ni pamoja na kufuta vibali vya kazi kwa baadhi ya waajiri wa kigeni, wakiwemo wa Hoteli ya Neptune ya Pwani Mchangani na Afrika House.

   Aidha mfanyakazi mmoja wa kigani wa Hoteli a Dolphine View ya Kizimkazi ambae pia alikuwa akilalamikiwa, kesi yake ipo Mahakamani kwa hatua za kisheria.

b) Mhe. Spika, pale inaptokea migogoro inayohusiana na mambo ya kazi, basi Wizara kwa hatua ya awali hujaribu kusulihisha mgogoro hiyo ili kulinda maslahi ya wazalendo na kukuza mahusiano mema kazini. Usuluhishi hufanya kwa kuzikiliza pande husika ili kubaini ukweli wa malalamiko hayo na baadae ushauri juu ya kutatua lalamiko husika hutolewa kwa mujibu wa sheria na sio kwa misingi ya upendeleo wowote ule. Iwapo pande husika hazijaridhika, basi shauri husika hupelekwa Mahakama ya Kazi. Katika utaratibu huu, hukumu la Wizara ni usuluhishi na katika usuluhishi hakuna upendeleo kwani iwapo pande husika haijaridhika basi fursa ya kwenda Mahaka ya kazi hutolewa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri una habari hivi karibuni kuna baadhi ya wananchi wamekatishwa mikataba yao na kupewa likizo bila ya malipo bila ya mkataba huo kwisha.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Sina habari Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala mola la nyongeza.

Mhe. Waziri unaweza kuliambia Baraza hili tukufu ni wafanyakazi wangapi katika mahoteli ya Zanzibar waliokuwepo katika mwaka wa 2010, ambao wamefukuzwa katika mahoteli yale kinyume na taratibu na wakaja katika serikali kuja kushtaki.Wakaendelezewa ile kesi na wakabainika kwamba wao walikuwa sio wakosa. Isipokuwa makosa yalikuwa ni ya wenye hoteli, lakini wao wakao wamerejeshwa makazini. Unaweza ukatupa takwimu ya wafanyakazi hao.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, wapo kweli waliofukuzwa, takwimu sasa hivi sina, lakini Ishaallah namuahidi nitamletea kwa maandishi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika kufuatilia tatizo hili muda mrefu kupitia Kamisheni ya Kazi, Wizara ya Wanawake na Watoto wakati huo. Ilionekana kwamba mikataba ilikuwa ina matatizo na kulikuwa kuna utaratibu wa kuanzisha mikataba mipya ambayo itaondoa mizozo.

Je, kutokana na Wizara mpya hii iliyoundwa na taarifa alizonazo, mikataba ipi inayotumika sasa hivi ni ile ile mikongwe au hiyo mipya ambayo ilikuwa inatayarishwa kuondoa mizozo ndiyo inayotumika sasa hivi. Ikiwa bado hiyo mipya haijatumika ni muda gani utakaochukua tena ili kupata mikataba ambayo haitaleta mizozo katika ajira za wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, kila muajiri anakuwa ana mkataba wake. Ni kweli kabisa kwamba mikataba ilikuwa ina matatizo makubwa. Mingi ya mikataba hiyo ilikuwa haimpi fursa na haki hasa yule mzalendo. Mara nyingi sana fursa zao zilikuwa zinanyimwa.

Hatua hiyo tumeichukua kwa Zantel, kulijitokeza matatizo wakati walipobadilisha mfumo wao, wafanyakazi wengi hasa wale wa kiwango cha chini kama walinzi na matarishi ambao walikuwepo pale hawakupata fursa ya marekebisho ya mishahara yao. Jambo ambalo tumechukua hatua, tumewaita na tumesema mikataba ile irekebishwe na tumeahidiwa pengine katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja marekebisho yao yatafanywa kwa hatua mbali mbali.

Hata hivyo Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Wizara yangu inafanya utarabu wa kuwa na mikataba ambayo ni *standard* kwamba mikataba hiyo iweze kusimamiwa vizuri na wote bila ya kutizama kampuni gani ina mkataba gani. Ni vizuri sisi kama serikali tuwe na mikataba yetu ambayo itafuatwa ili kuhakikisha kwamba wote wanapata haki kwa mujibu wa utaratibu ulivyo.

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mswada wa Sheria wa Kuanzisha, Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa Ajiri ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao Mengine ya Kilimo.

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa hii ya kujibu hoja za wajumbe na kuweka sawa kwa yale ambayo kuwa hayakufahamika yaliyokuwemo katika Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana wewe binafsi kuwa tangu jana kwa umahiri wako mkubwa uliokuwa nao. Unatoa fursa ya hali ya juu kwa wajumbe na sote katika Baraza hili juu ya kuchangia Mswada huu muhimu za ZSTC.

Pili nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia Mswa huu na kutoa maoni yao juu ya kuboresha Mswada huu tukianzia na:-

1) Mhe. Salmini Awadh Salmin - Mwenyekiti wa Fedha Biashara na Kilimo.
2) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3) Mhe. Rashid Seif Suleiman
4) Mhe. Asaa Othman Hamad
5) Mhe. Asha Bakari Makame
6) Mhe. Hemed Suleiman Khamis
7) Mhe. Bi Panda Ali Abdalla
8) Mhe. Saleh Nassor Juma
9) Mhe. Hassan Hamad Omar
10) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
11) Mhe. Mohamed Haji Khalid
12) Mhe. Abdalla Mohammed Ali
13) Mhe. Mussa Ali Hassan
14) Mhe. Rufai Said Rufai
15) Mhe. Hija Hassan Hija
16) Mhe. Abdalla Juma Abdalla

Mhe. Naibu Spika, katika kujibu hoja za waheshimiwa wajumbe naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi wa masuala yaliyoulizwa kwa kuanza na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa namshukuru kwa kuipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kumpa ushirikiano wa kukamilisha majukumu ya Kamati yake kwa ufanisi mkubwa. Pia natoa shukurani zangu za dhati kwake kwa kulizungumza kwa udhati kwa moyo wake, suala la magendo ya karafuu na kushauri hatua mbali mbali kwa lengo la kudhibiti rasilimali za nchi yetu.

Vile vile naipongeza kamati hiyo kwa kuona umuhimu wa kuimarisha utendaji wa Shirika la ZSTC kama wizara ilivyoona umuhimu huo. Pamoja na kuridhishwa na muundo na majukumu ya shirika. Mashirikiano ya Mwenyekiti na uongozi wake wa hekma alionao. Pamoja na ushirikiano wa wajumbe wake wote sisi tunauthamini sana na tunasema asante sana.

Mhe. Naibu Spika, tukianza katika ukurasa wa mwanzo wa Mswada huu yaani ukurasa wa 247 Mhe. Jussa Ismail, alikuwa ana wasi wasi na suala zima la kichwa cha habari cha Mswada huu. Napenda kumfahamisha kuwa kwa mujibu wa jina lililowekwa la ZSTC chini ya Mswada huu linalenga kufanyia masuala matatu makubwa. Nayo

1) Jukumu la kibiashara yaani *(Commercial functions)*
2) Jukumu la uhamasishaji *(Promotional functions)*
3) Jukumu la kazi za pamoja *(Shared functions)*

Kama iliyotajwa katika kifungu cha 7 cha Mswada huu, majukumu haya yameelezwa kwa ufasaha katika kifungu cha 7(1) masuala ya usarifu, karafuu, *blending* na vipi biashara ya karafuu itaendeshwa. Sisi tunaamini kwamba kifungu cha maeneo hichi kimekwenda moja kwa moja na maudhui ya Mswada huu.

Kuhusu ukurasa wa 248 suala la marekebisho ya kifungu cha 3 ikatafsiri maneno mjumbe iongezeke neno na baina ya bodi na jumuisha. Hilo tumelikubali marekebisho yake na tunaliunga mkono moja kwa moja.

Vile vile tafsi ya Waziri kusomeka isomeke waziri mwenye dhamana ya masuala ya kibiashara kwenye ukurasa 248. Hilo nalo tumelikubali moja kwa moja na tuliunga mkono lirekebishwe.

Katika ukurasa wa 249, kifungu 6 (2)(c) ushauri wa kufanya tafiti za mazao ya kilimo. Umo katika kufungu hicho lakini vile vile tunaupa umuhimu mkubwa kwa vile wajumbe wengi wamechangia kama Mhe. Asaa Othman Said, Mhe. Nassoro Juma, Mhe. Saleh Nassor na Mhe. Hemed Suleiman. Wote wametia mkazo suala hilo kwa hivyo na sisi tunalitilia mkazo na tunalifanyia kazi. Katika sheria imo katika kifungu 6 (2)(c).

Tukienda ukurasa wa 250 kifungu 7(1) kuhusu suala la bei ya ushindani, waheshimiwa wengi wajumbe wameonesha wasi wasi wao kuhusiana na suala la kipengele hichi kama Mhe. Jussa, Mhe. Rashid Seif, Mhe. Mohammed Haji Halid, Mhe. Saleh Nassor na wengineo.

Ningeomba niwafahamishe wajumbe kwamba katika kipengele hichi, Mhe. Naibu Spika, tunaposema kununua na kuuza karafuu na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani, hatukusudii ushindani wa ndani, tunakusudia ushindani wa nje. Kwa sababu ZSTC pekee ndiyo inayofanya biashara hii, lakini ni lazima ishindane na dunia nzima. Yaani wanaotoa mazao kwa mfano ya karafuu duniani. ni Madagascan, Comoro, Brazil, India, Sirilanka, Indonesia na kadhalika. Hapa ZSTC ni lazima iwe na ubavu wa kuweza kushindana katika masoko ya dunia na hapa ushauri wetu sisi ni kununua karafuu na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani. Yaani iweze kutoa bei ambayo kwamba itaweza kwenda kuuza nje na kushindana na wazalishaji wengine, sio ushindani wa ndani.

Katika kifungu cha 7(2) (h) kuhusu suala la maghala ambalo Mhe. Hija Hassan Hija alitaka aelezwe. Mheshimiwa sisi ZSTC hatujauza hata ghala moja, maghala yote ya ZSTC yamedhibitiwa kikamilifu hakuna lolote lilotokea katika maghala haya. Naomba nikuarifu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba maghala yote tuliyonayo ZSTC ni maghala 22 Unguja yapo 14 na Pemba yapo 8. Maghala haya mengine tunatumia

wenyewe na mengine tumewakodisha wafanyabiashara za chakula kwa muda mfupi mfupi, mwaka mmoja mpaka miaka miwili.

Unguja tuna *ware house*, Malindi tuna *ware house tatu*, Saateni kuna Lahakiba moja, Lahakiba mbili, Lahakitiba tatu. Kuna Saateni *godown copra* moja, Saateni *godown copra* mbili, Saateni *godown copra* tatu, Saateni *godown copra* nne, Saateni *godown cobra* tano. Kwa hivyo Saateni kuna kuna ma-*godown* matano ya *copra*. *Vision* la godown *seaweeds* moja la pili na la tatu.

Pemba tuna tuna Wete kubwa na mawili madogo Wete, Madungu Chake Chake, Kibirinzi Chakechake kina *warehouse* kubwa *Warehouse* moja Mkoani, *warehouse* la pili Mkoani, la tatu vile vile *warehouse* dogo na tuna *godown* moja la Kiwanda cha Makonyo *Distillery* Chake Chake. Kwa hivyo maghala yote haya yapo chini ya himaya ya ZSTC hakuna lililouzwa lakini yanakodishwa kwa kipindi cha muda mfupi kwa wafanyabiashara mbali mbali.

Katika ukurasa wa 252 kifungu cha 4 suala la *branding* Mhe. Jussa alikuwa amesema kwamba amevunjika moyo sana kwamba hakuona suala la *branding* katika Sheria hii. Nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa katika ukurasa wa 252 kifungu nam. 4, suala hilo limetiliwa mkazo kabisa kabisa, sual la *branding* halikusahauliwa. Madhumuni na maudhui hasa ya kuleta Mswada huu wa Sheria ili ZSTC iwe ni chombo chenye nguvu kwa sababu *branding* inahitajia pawepo na chombo ambacho kwamba kitaangalia ubora na kitaweza kutimiza masharti ya WTO kwenye suala la *branding*.

Kwa hivyo maudhui ya Mswada huu ni kuipa dhamana ZSTC na kuipa meno ZSTC ili isimamie suala hili la *branding* vizuri sana. Kwa hivyo katika ukurasa wa 250 katika kifugu 7(4)(f) suala la *branding* lipo na hilo ndio tumekusudia kwamba litafanya kazi hiyo. Kwa hivyo naomba Mhe. Jussa aangalie kifungu hicho atakuta suala la *branding*.

Vile vile kifungu Nam. 4 (h) tumepokea ushauri kutoka kwa Mhe. Panya habari ya elimu ya wakulima. Lakini katika kifungu hicho 4 (h) kipo kwa hivyo tunalichukua lote suala hilo.

Katika ukurasa wa 253 (9) kifungu nam. 7 na nam. 9 vinajirudia, Mhe. Rashid Seif alikuwa ana wasi wasi kuwa vifungu hivi vinajirudia. Lakini sisi Wizara inaona kuwa kuna mgawanyiko mzuri tu wa kazi katika shirika. Vifungu hivi ni vifungu viwili tofauti. Kifungu nam. 7 kinachambua kazi za ZSTC na kifungu nam. 9 kinatoa uwezo wa ZSTC kutokana na majukumu yake. Tunaomba Mheshimiwa avipitie vizuri vifungu hivyo aone kama kunatofauti, kuna kazi na kuna uwezo. Haya ni mambo tofauti na haya hayana uwiyana katika masuala mazima ya utekelezaji.

Katika kifungu Nam. 9 ufafanuzi juu ya suala la bei ya kununulia karafuu kulingana na bei ya kusarishia, ilikuwa kila nchi ina bei tofauti. Sisi kwa mfano tunauza karafuu kwa k utumia A4B Price. Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Jussa na Mhe. Rashid Seif walikuwa wana wasi wasi juu ya suala hili. Sisi tunapanga bei kwa kutumia *free on board (FOB).*

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu nam. 9(1) Mhe. Jussa ameonesha wasi wasi wake kuhusu kifungu hichi Mhe. Abdalla Juma, Mhe. Saleh Nassor, lakini naomba naomba niwaombe radhi kwamba kifungu hiki kimefutwa na Kamati ya Fedha ukurasa wa 4 umeonesha wazi kwamba kifungu Nam 9 (1)(f) kimefutwa na hakimo tena katika Mswada huu. Kwa hivyo nataka niwatoe wasi wasi kwamba kifungu hicho hakimo tena.

Kifungu nam. 10 (1) kuhusu uteuzi, mtendaji mkuu wa shirika. Suala hili Mhe. Jussa Ismail Ladhu, Mhe. Asaa Othman Said, Mhe. Rashid Seif, Bakari wote wameonesha wasi wasi wao. Mhe. Asha Bakari amesema Mhe. Rais tumpunguzie kazi, tunamtia aibu. Lakini kwa mujibu wa katiba yetu ya nchi ya Zanziba, inampa mamlaka Mhe. Raisi ya kuunda chombo na kuteuwa mtendaji Mkuu wa chombo hicho kwa mijibu wa Katiba yetu ya Zanzibar, nafikiri kifungu nam. 53.

ZSTC ni chombo cha serikali, bado ni sahihi kwa Mhe. Rais kumteuwa mtendaji mkuu wa chombo hicho, na pia kwa mujibu wa sheria wa mitaji ya umma inamtaka Mhe. Rais ndiye achague mkurugenzi

muendeshaji. Naomba mfanye marejeo katika sheria ya mitaji ya umma Nam. 6 (1) naomba niwasomee wajumbe

> ***Composition and proceedings of the board:***
> *The board shall consist of a chair person who shall be appointed by the president, such other the members including the chief executive officer being not less then five no more then seven members to be appointed by the responsible minister.*

Kwa hivyo ukiangalia kazi ya *proceedings* Rais ndio kapewa uwezo kwa mujibu wa katiba na kwa mujibu wa Sheria hii.

Vile vile Mhe. Jussa, Mhe. Rashid Seif, Mhe. Asaa na waheshimiwa wengine kwamba Kifungu Nam. 10 (4) kuhusu muda wa kikomo cha utendaji wa Mkurugenzi mtendaji. Tumepokea mawazo haya hili la mkurugenzi mtendaji kufanya kazi zaidi ya miaka 10 ikiwa utendaji wake hauna matatizo na sisi vile vile hatuna matatizo na tunawafikiana na wajumbe na tutasema kwamba inawezekana ikiwa yule mtendaji kafanya kazi zake vizuri. Kwa hivyo sisi tunawafikiana na mawazo yetu na tuko tayari kifungu hicho kukirekebisha na kwamba mjumbe huyo aweze kuendelea tena.

Tukiendelea kifungu Nam. 13(2) kuhusu mkurugenzi mtendaji asiwe mjumbe wa board. Suala hili kwa bahati mbaya haliwezekani kutokana na kuwa sheria madhali ya umma Kifungu Nam. 6(1) imeelekeza kuwa kiongozi huyo lazima awe mjumbe wa board. Sheria hii hapa naomba muangalie katika kifungu hicho, mtaona kwamba huyu anatakiwa atoke katika board.

Vile vile kifungu Nam. 18 kuhusu malipo ya posho la Wajumbe kuamuliwa na Waziri. ZSTC ni Shirika la umma ambalo kiutaratibu misingi yake ya kifedha inafuata taratibu za sheria ya mitaji ya umma.

Kifungu Nam. 10 (1) kwa mwenye sheria hiyo inatoa maelekezi kuwa waziri atakuwa anataratibu za wajumbe wa bodi. Mhe. Jussa hilo alilielezea wasi wasi wake. Ukisoma katika sheria hiyo ya *Public Investment Act* kifungu Nam. 10 inaitwa katika S*ection* ya *Numeration of the board*.

> "*The members of the board shall be paid such allowances as the board may with with pre consent of the responsible minister determined."*

Kwa hivyo kifungu hichi ndio kinampa madaraka Waziri kushirikiana nao na kupanga viwango. Na hii kwa sababu waziri, *board* inaweza kukaa ikajiwekea marupurupu makubwa zaidi ikajiwekea ma- *allowance* makubwa zaidi kuliko kuangalia mustakbali wa shirika na uwezo wa shirika. Kwa hivyo kwa mujibu wa kifungu cha sheria hiyo ya *investiment act* imempa mamlaka Waziri kupanga hivyo. Ni ushauri mzuri lakini hatuwezi kwenda kinyume na sheria ya *Investment Act.*

Vile vile katika ukurasa wa 256 Mhe. Abdalla Mohammed Ali kutoka Mkoani yeye amesema kwamba kifungu hicho kirekebishwe kinasema kwamba:

> "Mtu yeyote bila ya kibali cha Shirika atanunua karafuu ama Wizara ya Kilimo"

hapa anasema iwe atanunua au kuuza. Sisi hilo hatuna matatizo nalo, tumelikubali na tutaliingiza katika Mswada huu kwamba ni moja katika suala la muafaka kabisa.

Ukurasa wa 257 vifungu nam 23, 24 na 25 ambavyo Mhe. Jussa na wachangiaji wengine waliochangia kuhusu suala hili. Wizara yangu bado inafuata vifungu hivyo vya kisheria kuwa havina matatizo yoyote. Tunaomba waheshimiwa wapiti zaidi vifungu hivi waviangalie zaidi ya kupata maana halisi. Hakuna kanuni ambayo itatungwa kupinga sheria au kupinda sheria. Hakuna kanuni ambayo itatungwa kuwa zaidi juu ya sheria au iwe na meno zaidi ya sheria. Kanuni ni kitu ambacho kinatungwa kwa ajili ya kufafanua sheria katika sehemu ambayo inayohitaji ufafanuzi. Naomba hilo lifahamike kwamba pale imewekwa sio kwa sababu ya kupinga sheria. Ikiwa kanuni inapinga sheria basi sheria ndiyo inayofuatwa.

Vile vile Mhe. Abdalla Mohammed na mwengine anasema kwamba adhabu ya kifungo iondoshwe kwa sababu huyu anayekamatwa ni mkulima. Sisi tunasema kwamba adhabu ya kifungo ibakie ni muhimu sana. Bila ya hivyo magendo ya karafuu hayawezi kabisa kuondoshwa na si karafuu tu magendo ya aina yoyote yale.

Pia nataka niwaondoe wasi wasi katika utafiti tulioufanya tumegundua wanaofanya magendo sio wakulima. Wakulima wenyewe magendo hawafanyi, wanalima karafuu wanauza. Suala kubwa hapa anaefanya magendo ni mlanguzi. Kwa hivyo sioni mantiki ya wajumbe kuwaonea huruma walanguzi. Kwa sababu walanguzi ni wahujumu uchumi na ni wahujumu wa taifa zima.

Mhe. Naibu Spika, katika maoni ya jumla kulikuwa kuna maoni kutoka kwa Mhe. Jussa na Mhe. Salim wa Mtambwe kwamba bei ya karafuu tunaowapa wananchi ni ndogo sana kuliko bei iliyokuwepo katika soko la dunia.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikuthibitishie kwamba mimi nikiingia ofisini asubuhi kabla ya kufanya kazi yoyote kazi yangu kwanza ni kuangalia bei ya karafuu duniani na kuangalia bei ya mchele, sukari, unga na mafuta ya kupikia duniani, kila siku asubuhi ndio kazi yangu ya kwanza ninayoifanya katika ofisi yangu.

Kwa hivyo huu mtandao ninaoangalia mimi na mtandao wanaoangalia waheshimiwa wengine nafikiri labda ni mwengine. Naamini kwamba Mhe. Jussa mtandao umekucheza. Bei elfu 35 kwa tani bado duniani hakuna bei hi naomba nikuthibitishie hilo na mimi nataka niku *challenge* Mhe. Jussa. Mimi nataka uniletee mteja huyo, nitamuuzia karafuu tani elfu moja hivi leo, sasa hivi. Mhe. Jussa na wewe nitakupa *commission* ya dola milioni tatu sasa hivi ukiniletea mteja huyo tumuuzie karafuu kwa bei ya 35, nina hakika hapa tunaweza kumpa hata elfu 50 kwa kilo mkulima. Sisi hatujapata mnunuzi huyo na wala hatujamuona duniani kama yupo mnunuzi ambaye anaweza kununua karafuu kwa bei ya 35 kwa kilo.

Mhe. Salim yeye anasema kapata bei ya elfu 41 naomba uniletee mteja huyo na mimi nitanunua karafuu na wewe nitakula *commission* ya shilingi bilioni 4 na nitamuuzi karafuu tani elfu moja hivi leo. Naku *challenge* nasema kwa miguu miwili kwamba hakuna bei hiyo katika ulimwengu. Zote bei za karafuu ni hizi hapa mpaka leo asubuhi nimeziangalia. Naomba kuwafahamisha wananchi wote kwamba bei ya karafuu tunayowapa wananchi ndiyo bei halisi iliyotambulikana katika ulimwengu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kidogo unipe dakika mbili niwaelimishe wajumbe. Unaposikia kuna bei pahala kwa mfano mimi nilikuwepo Bangalore na India. Masoko matatu makubwa ya *spices* ni Bangalore, Delhi na Bombey. Mimi nilikuwepo Bangalore, nimekwenda kwenye soko la *spices* nikaona wanauza karafuu za Zanzibar kilo moja ni rupia elfu moja na ishini na tano kwa bei ya *hole sale* na kwa bei ya *retail* wanauza rupia elfu moja mia moja na hamsini. India rupia sasa hivi imeanguka sana, kama sisi hapa sasa hivi Tanzania shillings na Kenya. Kila siku rupia inaanguka tangu ilikuwa 44 per dola sasa hivi ni 52. Nikaangalia bei ya karafuu ya Bangalore tafauti na bei ya karafuu ya Bombay, tofauti na bei ya karafuu ya Delhi, tafauti na bei ya Culkata ni nchi moja lakini *logistics* zina *change price from place to place*.

Vile vile unapoambiwa karafuu inauzwa India. Kwa mfano India karafuu inauzwa tani moja dola elfu 20 kwa mfano. Kwa hivyo usifikiri bei hiyo wewe Zanzibar utauzia bei hiyo, hakuna. Mimi nimekwenda Bangalore nimefanya utafiti nimeona kwamba Bangalore kwanza kuna *custom duty* ya *fourteen percent* imelipwa kwa karafuu zile kwa bei hiyo. Pili kuna VAT ya 5% inalipwa kwenye bei hiyo. Kuna *miscellaneous charges 3*.5%, kuna 2% *sales commission*, kuna *profit margin* wanayoiweka pale ni 6.67 nimeangalia kuna *handling, freight, insurance* na kadhalika. Kwa ufupi wana 26% to *the basic price, to the big price, depending apon logistics.* Kwa hivyo Bangalore bei yao wao ukiuza karafuu hapa uengeze 26% ndio karafuu ile bei ya Bangalore, ukenda Delhi imezidi zaidi, ukenda Calcatta imezidi zaidi. Kwa hivyo bei ya Singapore bei ya Indonesia, bei ya Amerika, bei ya Canada, bei ya London karafuu haiwezekani kuwa sawa sawa kwa sababu ya *logistic. Is one Country India* kuna *three prices* tofauti ya Delhi ya Bombay na ya Bangalore.

Nilipokwenda mimi kule Bangalore karafuu inauzwa kilo moja rupia 125, hiyo ina maana tani moja ni dola 20,500. Lakini ukitoa gharama zote hizo nilizokwambiani inakwenda *sixteen thouth an per ton* na bado hajaingiza faida yake yule muuzaji. Kwa hivyo, tusifikirie tu tukenda katika *google* tukatoa *price* ya

karafuu tukaona imeandikwa hiyo ukaona wewe Zanzibar utapata hiyo. Kwa kweli hupati hiyo hapa sisi tuna *A for B price* ambayo tunamuuzia mtu karafuu ghala ya Malindi pale anaisafirisha anaipeleka nje.

Mhe. Naibu Spika, naomba radhi kwa kupoteza wakati lakini nataka niwafahamishe wajumbe ili wasije wakawapotosha wananchi, wananchi wakaona serikali yao inawadhulumu na serikali yao haisemi kweli. Rais wa Zanzibar ametamka tamko hili kwa udhati kabisa na mimi waziri natamka hivyo hivyo kwamba tutawapa wananchi asilimia 80 ya *export price* yetu tunawauzia karafuu. Hili hatuna hiana kwa wananchi tumesema wazi kabisa na wananchi wasiwe na wasi wasi na tumetoa ahadi bei ikishuka sisi tunachukua dhamana juu ya suala hilo. Mhe. Naibu Spika, tena nawaambia ndugu zangu Wajumbe na wananchi mna wasi wasi gani na serikali yetu, na serikali imejidhatiti suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *ZSTC* kuwa na ofisi au mwakilishi nje ya Zanzibar, serikali katika jitihada zake za zao la karafuu na mazao mengine ili liweze kutoa tija kuwa kwa wakulima na nchi kwa ujumla imeweka mkakati maalum wa kisoko ambao umeelekeza katika utumiaji wa *branding IPZ capture* ili kuweza kupata ili kuweza kupata angalau zaidi ya asilimia 50 ya bei ya mwisho. Mhe. Naibu Spika, tafiti zimefanywa kwa mazao ya kilimo zimebaini kuwa wakulima wamekuwa wanapata chini ya asilimia 5 ya bei ya mwisho, kwenye karafuu mkulima anapata *5 percent* ya bei ya mwisho. Lengo kuu la afisi hii ni kuwa na uwakilishi na kuwa na mahusiano ya karibu na soko la bidhaa zetu ili kuweza kuleta thamani ya mwisho ya bei ya mtumiaji.

Kwa dhamana hizi ambazo *ZSTC* tunataka kuwapa halafu tukawa limit kwamba wao lazima watoe uwakilishi hawawezi kufungua afisi naamini kwamba itakuwa tumeitia ujamu *ZSTC* isiendelee mbele. Kwa hivyo, hapa kama *necessary* afisi itafunguliwa, kama sio *necessary* afisi itaondoshwa.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunafanya *study* ya kutosha kwenye Shirika la *ZSTC*, tunaingilia afisi moja moja tunaiangalia kwa mfano ikiwa Afisi ya Dubai tunaona haina maslahi basi itafungwa. Mhe. Naibu Spika, hatufunguwi afisi kwa sababu ya *just waste money* tutafungua afisi *whan its necessary*. Naomba hilo wajumbe wasiwe na wasi wasi.

Mhe. Naibu Spika, mtendaji mkuu nimeshaeleza kwamba sisi hatuna wasi wasi wowote kwamba mtendaji mkuu anaweza kukaa hata dakika 20 kama atakuwa anafanya kazi zake vizuri, hilo hatuna wasi wasi wowote. Kuna wajumbe wamesema kwamba karafuu zao hili ni la wenyewe, mbona nyinyi mnaling'aninia kwa nini hamliachii zao hili, mnaling'aninia hamtaki kulitoa bora mliachie liwe huru.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawaambia ndugu zangu wajumbe kuna *body guard* mmoja alimuuliza Mhe. Mandela asubuhi walikuwa wanakwenda *working* katika mazoezi, Mandela akamuuliza yule *body guard how is the family* akamwambia familia yangu iko sawa. Na yule *body guard* akamuuliza Mandela *what about the family* akamwambia *I have a large family fourtyfour milion people.* Kwa hivyo, hapo unapozungumzia karafuu, karafuu tumeshasema kwamba sera yetu ni karafuu ni zao la taifa. Kwa hivyo, karafuu sio ya mtu mmoja, karafuu ni yetu sote hata yule ambaye hana mkarafuu basi karafuu ni yake.

Mhe. Naibu Spika, tunampa yeye yule anayeshughulika na karafuu tunampa *8 percent* lakini tuna *20 percent* ya Wazanzibari wengine na kuna *other benefit* zinaweka katika zao la karafuu. Kwa hivyo, karafuu ni zao la taifa na sio zao la mtu mmoja mmoja, na hii ndio sera ya nchi na kila nchi ina sera hiyo. Botswana wana almasi, Gulf huko kuna mafuta kila nchi imeweka zao lake fulani kuwa ni zao la taifa na ni zao la kiuchumi. Kwa hivyo, sisi tukisema kwamba Zanzibar hatuna zao la kiuchumi itakuwa hatuna *strategy*. Kwa hivyo, tunaomba wajumbe wafahamu kwamba suala la *protect* karafuu sawa ni zuri, lakini lina wakati wake na lina mikakati yake.

Mhe. Naibu Spika, sisi kwanza tumeona jambo la kwanza ni kuweza kuimarisha Shirika la *ZSTC* ili liweze kusimamia vizuri suala la karafuu na mazao ya karafuu na mikarafuu wenyewe. Karafuu ilikuwa inazaliwa tani 25 kwa mwaka sasa hivi ni tani 3000, huko unapotaifisha karafuu sasa hivi ukafanya kila mtu tena afanye atakavyo kuna hatari zao hili kuondoka katika mandhari ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tunaamini kwamba kwa mikakati tuliyoiweka karafuu tunataka iweze kuongezwa kutoka tani 3000 mwaka huu mpaka miaka 10 ifike tani 15,000. Madagascar karafuu ziko huru, Comorro

karafuu ziko huru, Brazil karafuu ziko huru, lakini *quality* yake ni mbaya ukilinganisha na karafuu ya Zanzibar. Na wote wale wanao nunua karafuu wanasema siku karafuu mtakapoibinafsisha Zanzibar mjue *quality* ya karafuu Zanzibar itakuwa siku hiyo mmeshaimaliza. Kwa hivyo, suala la karafuu kubinafsisha inataka ifikiriwe sana.

Mhe. Naibu Spika, sisi kwanza tuna malengo kumpa mkulima nyenzo na kumpa mkulima nafasi kubwa sana ya kupata mapato makubwa, lakini pili kuimarisha karafuu zizalishwe kwa wingi kutoka tani 3000 kwenda tani 10,000. Vile vile kuitia *branding* ili karafuu isiuzwe kwa magendo na iwe na jina. Kwa hivyo, zote juhudi hizo hatuwezi kuzifanya ikiwa tutabinafsisha, tukibinasisha kesho ina maana *branding* tuisahau, ina maana tuache kuwapa wakulima asilimia 80 na tuache kuweka mfuko *CDF* wa maendeleo ya karafuu. Naamini kwamba kwa huu mkakati tulionao sisi utakuwa ni sahihi kuliko kubinafsisha zao la karafuu, hatung'anini kwa sababu ya kumkomoa mkulima, la hasha! Tunang'aninia kwa sababu ya kujenga uchumi wa Zanzibar, uchumi wa Zanzibar ukiinuka ni mafanikio kwa Wazanzibari wote. Uchumi wa Zanzibar ukiporomoka ni janga kwa Wazanzibari wote.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane kwamba tunataka kwa kila hali kulifanya zao la karafuu kuwa la kiuchumi na kwa manufaa na maslahi ya wakulima na maslahi ya taifa zima. Mhe. Naibu Spika, *ZSTC* vile vile haikusudii kumtoza kodi mkulima yeyote katika kituo, Mhe. Salim amesema kwamba kule Mtambwe katika vituo kuna watu wanatozwa pesa. La hasha! *ZSTC* haitozi pesa mtu, anapokwenda katika kituo muuza karafuu ni wajibu wake mzigo ule aubebe kutoka kwenye gari mpaka kwenye mezani, ukishafika katika mezani mzigo ule ukishapimwa sio wake tena ni wa *ZSTC* pale *ZSTC* ndio una jukumu la kuubeba na kuutia katika ghala yake.

Mhe. Naibu Spika, lakini leo muuza karafuu kenda na mzigo wake tangu kwenye gari anataka abebewe bure, amiminiwe chini, anyambuliwe taka taka, apelekwe kwenye mezani bure, hili haliwezekani. Mhe. Naibu Spika, hayo mazungumzo hayo afanye mwenyewe mkulima na mchukuzi *ZSTC* haihusiki, ikiwa mkulima hataki mzigo wake abebewe basi abebe mwenyewe asimpe mchukuzi, akimpa mchukuzi lazima amlipe. Mhe. Naibu Spika, ukenda katika meli ukimpa mzigo mchukuzi si unamlipa, ukenda ukichukua saruji katika ghala au sukari au unga mchukuzi si unamlipa.

Kwa hivyo, kwa nini muuza karafuu anamzulia *ZSTC* kama inatoza pesa ni kwamba *ZSTC* haimtozi mtu uchukuzi, uchukuzi ni baina ya mchukuzi na mwenye karafuu. *ZSTC* ikishakuwekwa gunia katika mezani kuanzia hapo mchukuzi huyo analipwa na *ZSTC*, lakini kutoka kwenye gari mpaka kwenye mezani ni suala la mwenyewe mkulima. Kwa hivyo, akakae kitako kwa makini asikilizane bei na mchukuzi kwamba mzigo wangu unauchukua nitakulipa kiasi kadhaa, mzigo wangu usiuchukue nitabeba mwenyewe mpaka kwenye mezani.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu bodi kuwa na zaidi ya wajumbe asilimia nusu, Mhe. Jussa suala hili alikuwa na wasi wasi nalo. Lakini nataka nikuhakikishie Mhe. Jussa sisi hatuna chochote ni lugha tu, tukisema zaidi ya nusu katika bodi hii kuna watu 9 haiwezekani kuwa katika watu wale 9 tutamkata mtu mmoja awe nusu. Kwa hivyo, tukiwa nusu maana yake ni watu 5 na watu 5 maana yake ni zaidi ya nusu, kwetu sisi suala hili hatuna lolote ikitaka lugha kurekebishwa tutarkebisha lakini lugha hii haina matatizo yoyote zaidi ya nusu itakuwa ni watu 5.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuhusu kuchukua wafanyakazi kutoka serikalini, mheshimiwa amesema kwamba tunachukua wafanyakazi kutoka serikalini wakati kuna watu tayari wameshawekwa kuna vijana huko mitaani wamemaliza maskuli hawana kazi. Naomba nimfahamishe Mhe. Salim Abdallah Hamad kwamba kwanza tunapunguza gharama, unapomchukua mfanyakazi wa serikali hatumpi mshahara tunampa posho tu kama tunavyowapa wale wafanyakazi wetu. Vile vile wafanyakazi tunaowachukua kule sisi wafanyakazi wenye uzoefu wa zile kazi, sio tunachukua mtu barabarani tukamuokota tukamtia kwendaa kufanya kazi ile.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili tunataka usalama wa mali zetu, huyu mfanyakazi wa serikali ameshafanya kazi katika serikali miaka 15 au miaka 20 ana haki zake katika serikali akenda akifanya ubadhirifu katika vituo atakosa haki zake zote hizo. Lakini mtu ukimuokota njiani akija pale anaweza akaondoka na bunda la pesa, anaweza akaondoka na polo la karafuu humuoni tena na huna pakumkamata, utamkamata wapi. Kwa

hivyo, kwa kuzuia hayo ndio tunachukua watu ambao kwamba wana *experience*, watu ambao wana dhamana kama pakitokea kitu unapo pakwenda kumkamata na kumchukulia hatua.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la mashamba ya serikali kweli, kuna mashamba ya serikali ya mikarafuu nakubaliana na ushauri wa wawaheshimiwa kwamba mashamba ya mikarafuu kwamba hayaangaliwi na wale ambao wamepewa eka basi wanyanganywe wapewe watu wengine. Lakini hii sisi sio kazi yetu ushauri huu tutauchukua tutaupeleka katika wizara inayohusika kwa kufanyiwa kazi.

Vile vile kuna wajumbe wengi wanung'unika, wametoa ushauri hapa kuhusu habari ya karafuu mbichi, karafuu kazi kusafirisha kutoka pahala kupeleka pahala pengine na mambo mengine. Kuhusu masuala haya kimsingi wizara haifanyi makosa inayatekeleza maelekezo ya sheria Nam. 11 ya mwaka 1985 kifungu cha 7(2) na kifungu cha 4(1) vifungu hivyo kwa pamoja vimeeleza taratibu na masuala ya uwekaji wa karafuu kama hivi ifuatavyo.

"No person shall store his cloves in house or at any other place. No, person shall move un dried clove, mother of cloves or cloves from one area to another".

Hii jamani ni sheria kwa hivyo sisi hatuwezi hata kidogo kupingana na hizi sheria, kwani hizi sheria ipo inafanyakazi na ndio maana ukaona watu wanapekuliwa wanaoweka karafuu na watu wengine wanazuiwa. Naomba muwe na subra sheria ya karafuu inatayarishwa mwezi wa Januari itakuja mtachangia na sheria hiyo mtashirikishwa na mtachangia. Kwa sasa hivi hii sheria ni ya *ZSTC* sio sheria ya karafuu, kwa hiyo unapochangia sheria ya *ZSTC* masuala ya karafuu ni kinyume nyume. Kwa hivyo, naomba muwe na subra mwezi wa Januari *inshaallah* tunatayarisha hapa mswada wa sheria ya karafuu, yote sisi tumeyaona na malalamiko tumeyachukua na tutayaingiza katika mswada huo na tutakuja kujadili hapa na tutafikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mazao yepi ya kilimo yatakayoshughulikiwa na *ZSTC*. Katika sheria kifungu cha 26 cha mswada huu waziri kushirikiana na wadau na ataamua ni mazao gani yaingizwe katika mazao ya kilimo. Waheshimiwa Wajumbe musiwe na wasi wasi hiyo sheria iliyopita ya *ZSTC* ilikuwemo suala hilo, na sheria ya *CVA* hii hapa iliyoundwa mwaka 1934 ilikuwemo hiyo mazao ya karafuu na mazao mengine ya kilimo. Kwa hivyo, hili sio jipya lipo tangu mwaka 1934 kwenye sheria ya *CVA* ambayo ni hii hapa hilo suala limo na halina utata wowote lina *very good experience*.

Mhe. Naibu Spika, tutakapoona kwamba Mhe. Hija amesema kwamba manjano inatoka katika jimbo lake tuitia katika orodha tukiona haina tatizo tutaitia katika orodha. Pia alisema pilipili hoho ikiwa nayo tunahisi itiwa katika orodha nayo tutaitia katika orodha. Kwa hivyo, hili lisitutie wasi wasi sio suala la ndizi, si suala la embe ni suala la orodha ya mazao ya kilimo ambayo tutahisi yatakuwa na soko katika dunia na hili waziri atashauriana na wadau wote.

Mhe. Naibu Spika, serikali tayari imeshaweka taratibu zake kuhusu habari ya chakula, hili tuwaachie Wizara ya Kilimo tutaishughulikia. Kuhusu uteuzi wa viongozi watatu katika shirika, mabadiliko ya muundo wa shirika yanategemea mazingira yaliyopo kwa hiyo ni busara kuachia bodi kuzingatia suala hilo kama kifungu Nam. 11 (a) cha mswada kinavyoeleza. Naomba wajumbe hili walikubali.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu muhimu wa teknolojia na utafiti pendekezo hili sisi tunalifurahia sana la wajumbe kuhusu umuhimu wa kuwa na teknolojia ya kisasa na tafiti mbali mbali juu ya zao karafuu na mazao mengine ya kilimo. Kuhusu *ZSTC* kutoa mikopo ya ulimiaji wa masuala ya mikarafuu Mhe. Naibu Spika, mswada huu wa sheria unazungumzia *ZSTC* kama chombo, kuna sheria ya karafuu nayo, kuna mfumo wa karafuu utakuja masuala yote haya yanaelezwa. Naomba muwe na subra ikifika siku mtatuchangia.

Mhe. Naibu Spika, pia yakiwemo masuala ya mikopo kwa wakulima wa karafuu kwa ajili ya kutayarisha mashamba yao yamo katika mswada huo huo wa sheria ya mfuko wa maendeleo ya karafuu. Kwa hivyo, nawaomba waheshimiwa muwe na subra kwa sasa hivi shirika linatoa mikopo kwa ajili ya kusaidia shughuli za uvunaji karafuu tu, sio kwa sababu ya shughuli ya kulimia mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, kuna wengine wamesema kwamba *ZSTC* haijahamasisha wananchi juu ya suala zima la karafuu. Mhe. Naibu Spika, katika wizara yetu wananchi wamehamasika sana na suala la karafuu kwa ujumla, hivi sasa kila mmoja anasafisha mashamba yake na kwa kweli mashamba ya mikarafuu sasa hivi mengi yako safi, vitalu vingi vimeimarishwa vya miche ya mikarafuu na wananchi kwa kweli wamehamasika sana juu ya masuala ya karafuu. Kwa hivyo, sisi tuna imani kwamba wananchi wamehamasika kwa kampeni na mambo mengine. Kwa hivyo, kwamba *ZSTC* haihamasishi kikweli, tunahamasisha na wananchi wamehamasika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la vitalu vya mikarafuu ni kwamba Wizara ya Kilimo imeshatuahidi kwamba itatoa mikarafuu 500,000 kila mwaka, kila msimu wana vitalu watatoa mikarafuu 500,000 kwa ajili ya kuhamasisha wakulima. Kwa kweli mikarafuu itakuwa ni bure mkulima hauziwi atapewa bure atakwenda kupanda na vile vile kutakuwa na washauri mbali mbali kutoka Wizara ya Kilimo watayapitia mashamba hayo ambayo yatapandwa mikarafuu hiyo. Mhe. Naibu Spika, vile vile vitalu mbali mbali vya watu binafsi vimehamasika katika kupanda miche ya mikarafuu na hili ni jambo la kutia moyo sana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kushirikishwa jumuiya za mikarafuu, naomba kuwaambia kwamba katika waraka huu basi nafasi mbili, moja kutoa Unguja na moja kutoka Pemba watashirikishwa katika Bodi ya *ZSTC*. Vile vile kulikuwa kuna suala hapa kwamba *ZSTC* itashughulikia vipi wale ambao kwamba walioanguka katika mikarafuu. Vile vile suala hili tunajua ni suala gumu na ni kubwa na hili tumelitia vile vile katika sheria ile ya karafuu. Lakini kwa sasa mtu yeyote ambaye kwamba amejeruhiwa kutokana na kuanguka kwa mkarafuu tunamshughulikia mpaka kupona kwake, lakini katika sheria ijayo tumeichanganua vizuri sana na mtaichangia vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, uwezekano wa kutumia njia ya kisayansi ya kukaushia karafuu. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwafahamishe kwa ufasaha kabisa ni kwamba karafuu tunazitia katika magunia yale sio kwa hiari zetu, karafuu zile kwa maumbile yake zinatakiwa zitiwe magunia yale. Ndio soko linavyotaka kwa sababu karafuu inatakiwa iwe na viwango, inatakiwa isizidi *fourteen percent moisture*, karafuu ukiitia ndani ya mfuko wa *plastic* au kipolo *moisture* yake inaongezeka inafika mpaka 30 kwa hiyo karafuu itakosa soko itavimba itakuwa haifai katika soko.

Katika soko kuna viwango wenyewe wameviweka hao wanunuzi wa karafuu wanasema kwamba *not more than four percent of stem mother clove of a sort matter four percent of local clove not more than fourteen percent moisture*. Karafuu tunapotia katika magunia yale yenye tundu tundu yanatoa mvuke nje kwa hivyo karafuu zile hazipati mvuke, kwa hivyo hazipati *moisture* na ndivyo wanavyotaka wenyewe hao wanaonunua karafuu. Na mwenyewe masharti yake anakwambia huyo mnunuzi anakwambia karafuu yangu *packing* yangu ninayotaka nataka itiwe katika magunia mawili zenye uzito wa kilo 40.

Kwa hivyo, ukitaka wewe tutia kilo 20 mwenye kununua hataki itakuwa ni matatizo, ukataka wewe tutie kwenye mfuko wa plastic mwenye kununua hataki itakuwa ni tatizo. Kwa hivyo, musione sisi tunatia katika magunia mkafikiri kama sisi tuna mambo ya zamani, ila hiyo ndio *demand* ya wanunuzi karafuu ili ifike inapokwenda itiwe katika gunia linaloruhusu hewa kuingia na kutoka. Vile vile kuna wengine wanataka karafuu ikaushwe katika mitambo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hivi juzi kule Wete kaja mtu kaja kuuza karafuu amezikaanga amezileta kuziuza. Mhe. Naibu Spika, sisi *ZSTC* na dunia nzima haitaki karafuu iliyokaangwa, hawataki karafuu iliyochakatuliwa, karafuu ukikausha kwa njia nyengine yoyote ambayo sio jua basi umeichakachua na kwa namna hiyo haipati bei wala haipati soko. Kwa hivyo, bado nasisitiza kwamba karafuu inakaushwa kwa jua ndio karafuu ya mwanzo inayotakiwa katika ulimwengu huu, karafuu yoyote nyengine inayokaushwa kwa njia nyengine isiyokuwa ya jua ni kuichakachua na kwa hivyo haina soko wala haitakiwi.

Kwa hivyo, sisi Zanzibar karafuu yetu bado ina soko kubwa kwa sababu tunaianika katika majamvi, tunaianika kwa jua hatuichakachui na ndio maana ikawa ina soko zuri. Kwa hivyo, hakuna teknolojia nyengine nzuri zaidi kuliko hii, kwamba karafuu ianikwe katika jua la kawaida sio kutumia *solar* hiyo ni kuichakachua na haitakiwi kwani inapunguka viwango vyake vya ubora na haitopata hiyo bei tunayoitaka.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid alikuwa na wasi wasi lakini nataka nimjibu kwamba hoja yake shirika halikuwa limewezeshwa kwa sheria bali limewezeshwa kwa *legal notice*. Hii *ZSTC* hapo mwaka 1968 haikuanzishwa kwa sheria ilianzishwa kwa *legal notice* ambayo tangazo la kisheria sawa na kanuni ndio maana tukasema vile. Kwa hivyo, ile ni *legal notice* sawa na kanuni sio sheria, kwa hiyo usiwe na wasi wasi kwamba sisi tumeunda sheria.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Khalid akasema kwamba hata kama sheria ilikuwepo bado kwa vile ingefutwa na sheria hii mpya inabidi itamkwe hivyo, hata kama ile ingekuwa ni sheria inabidi tutamke vile. Kwa hivyo, hilo namuomba mheshimiwa lisimtie wasi wasi na chini ya sheria hii ya *ZSTC* hivyo sheria lazima ieleze kwamba kanuni ile inafutwa, sawa jamani itakuwa hiyo haitumiki tena.

Mhe. Naibu Spika, naamini baada ya maelezo hayo wajumbe wote wameridhika nimejaribu kujibu hoja zote japo sijamaliza lakini angalau asilimia 50 nimefikia, na rai zote zilizotolewa na wajumbe hapa naamini kwamba wajumbe wataunga mkono juhudi zangu binafsi na juhudi za wizara yangu na juhudi za Rais wa Zanzibar na juhudi zote za serikali juu ya kuona zao la karafuu ni zao la kimataifa la kumkomboa mkulima, na kumkomboa Mzanzibari. Kwa hivyo, naomba wajumbe wote mkubaliane na mswada huu tuupitishe ili nchi yetu iimarike kiuchumi. Ahsante sana naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaoafikiana na hoja ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wanyanyue mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

SEHEMU YA KWANZA – UTANGULIZI

Kifungu cha 1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2	Kutumika
Kifungu cha 3	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA PILI – KUANZISHWA MALENGO NA KAZI ZA SHIRIKA

Kifungu cha 4	Kuanzishwa kwa shirika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 5	Muhuri wa Shirika
Kifungu cha 6	Malengo ya Shirika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 7	Kazi za Shirika pamoja na marekebisho yake

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina kuhusiana na masuala mbali mbali ambayo tumeyaibua katika mjadala huu.

Katika kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema kuna marekebisho machache ya lugha ambayo nilisema nitayataja wakati wa kupitisha vifungu kutokana na kwamba ni mambo madogo madogo. Naomba niyataje ambayo naona kidogo yananipa shida kutokana na yalivyotafsiriwa na bahati mbaya mengine katika marekebisho ya kamati yalikuwa yameachwa.

Moja Mhe. Mwenyekiti, ni katika kifungu cha 7(2)(e) pale ilipoanza limetumika neno ‘kubadilisha biashara na kuendeleza malighafi’. Ukiisoma ya Kiingereza inazungumzia, *exchange trade and develop resources.* Sasa ile *exchange* na *trade* ni maneno mawili tofauti, lakini hapa yametafsiriwa kama vile *exchange* zaidi

ni kubadilisha biashara. Kwa hivyo, inabadilisha maana, nadhani kama tunakusudia *exchange* ni ubadilishaji basi tungeandika ubadilishaji, biashara ili ikaleta maana yake iliyokusudiwa.

Halafu katika kifungu cha (h) Mhe. Mwenyekiti, vile vile hata yale masuala yaliyoibuliwa na baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako jana yalikuwa yanatokana na tafsiri isiyo sahihi ya Kiswahili juu ya maneno yaliyotumika katika Kiingereza. Kwa mfano, ukisoma kifungu cha (h) katika Kiingereza panapozungumzwa *storage and stocking in warehouses,* sasa huku utakuta imetafsiriwa kusambaza vifaa vya usimamizi, pale pamezungumzwa *supply chain management facilities*. Sasa nilikuwa nasema sijui kama itakuwa ni kusambaza huduma za usimamizi ndio sahihi zaidi.

Lakini kuna maneno vile vile pale yametumika 'majengo na utengenezaji wa vituo vya kuuzia na maghala'. Ukisoma Kiingereza inasema *Building and maintenance of buying posts and warehouses*, yaani kujenga hivi vituo sio majengo. Sasa nadhani Kiswahili ingekuwa ni ujenzi na utengenezaji wa vituo vya kuuzia na maghala.

Halafu pale katikati kumeingia neno katika mstari wa pili kutoka chini, kuweka katika maghala halafu maneno gharama za huduma. Kwa hivyo, neno 'gharama za' nadhani linapaswa liondoke kwa sababu linapotosha maana iliyokuwepo pale. Mhe. Mwenyekiti nadhani kwa kifungu cha 7 niishie hapo kwanza.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 7 cha (e) na (h) mawazo ya mjumbe muwafaka.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante mawazo yamechukuliwa na kifungu kimekubaliwa.

Kifungu cha 8 - Kukasimu madaraka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 9 - Uwezo wa Shirika pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Salim Abdalla Hamnad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nasimama hapa nikiwa natamaa ya kupata shilingi bilioni nne kutoka kwa Mhe. Waziri na nitashirikiana kikamilifu na Mhe. Ismail Jussa tuone kuwa hizi pesa tumezitia mfukoni.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi sijasikia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nasema Mhe. Mwenyekiti, kwanza nasimama hapa kwa furaha ni kuwa nina tamaa ya kupata shilingi bilioni nne na rafiki yangu Mhe. Ismail Jussa shilingi bilioni tatu na tutashirikiana hizi pesa tuzitie mkononi kama Mhe. Waziri alivyotuelekeza.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki cha 9(b) kupanga bei ya kununulia karauu na mazao mengine ya kilimo. Mimi nilisema hapa kuwa mkulima anapopeleka karafuu zake na bei keshapangiwa kwa hivyo matarajio yake ni kupata ile bei aliyopangiwa, lakini kuna mchezo unachezwa katika vile vituo. Ukiiangusha tu ile gunia ya karafuu mle katika vituo haipelekwi kwenye mizani mpaka kwanza imiminwe, iangaliwe, anayepanga *grade* apange ikiwa ni chafu kila mtu aangalie kuwa hii sasa ni tayari kwa kupimwa na kununuliwa ndio tena ipelekwe kule kwenye mizani.

Sasa inapotoka kwenye gari mpaka ikaingia mle ndani pale inapomiminwa kuna wapagazi wanaochukua pale mpaka kwenye mizani sio mwenye mali na wale ni lazima wachukue wao na wao wanadai shilingi elfu tano kwa gunia. Hili ndilo nililosema. Sasa ikiwa Mhe. Waziri hajaipata hii basi hiyo nampa ni rasmi, hivyo lile suala la kuwa ni juu ya mwenyewe kupeleka kwenye mizani huko tunakouza karafuu haiko, karafuu kutoka ndani ya banda la kununulia karafuu na kupeleka kwenye mizani ya wale wafanyakazi walioajiriwa ni ile Shirika la *ZSTC* kwa hivyo hutaka uwalipe malipo pale ya lazima japokuwa mwenyewe unaiweza. Hilo ni moja.

Pili hapo hapo, nilisema kuwa kuna huyu mtoa fedha kila unapopeleka karafuu zako gunia moja huwa anakata shilingi elfu moja iliyokuwa haina maelezo. Hii nimeipata katika kituo cha Bwagamoyo na jana aliyehusika nilimpigia simu kwa kumdadisi mara kwa mara na akasema hili ndilo linalotendeka. Kwa

hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri kwa hili alitolee taarifa rasmi, vipi utaratibu uwe kwa sote ili pasipite mambo ambayo ilikuwa yasitendeke.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimfahamishe Mhe. Mjumbe kwamba suala analozungumza hilo rais ametembelea katika vituo vya kununulia karafuu, Makamo wa Kwanza wa Rais ametembelea mara mbili, mimi nimetembelea na naibu waziri wangu ametembelea hivi wiki mbili zilizopita. Makamoa wa Kwanza wa Rais ametembelea wiki moja nyuma na malalamiko hayo yameelezwa na wananchi katika vituo hivyo. Makamo wa Kwanza amewafahamisha kwa ufasaha kama nilivyokufahamisha mimi hapa.

Mhe. Makamo wa Kwanza kenda kituo kwa kituo na kila kituo alichokwenda kawaeleza kwamba, suala la kuchukua karafuu kutoka kwenye gari mpaka kwenye mizani ni wajibu wa mwenyewe mkulima, akitaka kumpa shilingi elfu kumi, elfu moja, milioni ni yeye na mkulima. *ZSTC* inakuwa pale kutoka kwenye minzani kuingiza ndani.

Shilingi elfu moja hiyo jana ulipozungumza wewe mimi usiku ule ule nilitoa kazi kutaka kujua nani anawatoza watu shilingi elfu moja, sisi ndio kwanza tumeisikia jana hiyo. Hili linafanyiwa kazi naamini kwamba ikiwa itakuwa sio *ZSTC*, lakini kama kuna mtuo yeyote anachangia mtu shilingi elfu moja ambaye hatoki *ZSTC* tutamkamata na tutampeleka katika vyombo vya sheria huyo atakuwa anaiba. Sisi *ZSTC* hakuna mpango huo.

Suala la wachukuzi wetu kutoka ZSTC kuna suala moja, tatizo kuna watu wengine wanakuja na karafuu pale katika mifuko yao wanatia mawe na michanga, tena watu wastahiki tu, wengine watu wakubwa, wengine mashekhe. Karafuu zishapimwa anatia mkono anatia jiwe. Kwa hivyo ndio tukawataka wachukuzi wetu sisi ndio wachukue kutoka kwenye mizani kwa sababu pale kwenye mizani ni pahala pa kuhushi, watu wanatia mawe.

Wakati wa kumimina karafuu kule Mkoani linatoka jiwe katika gunia la kilo tano au kumi, hayo wanafanya wakulima ndio tukasema wachukuzi wa pale lazima wawe wote wanajulikana. Kwa sababu ikiwa jiwe limeonekana katika gunia la karafuu tukimkamata mchukuzi tutampeleka polisi ndiye atakayehusika, lakini mazungumzo ya bei baina ya wewe na mchukuzi. Baada ya kusema hayo nasema kwamba suala lake linajulikana na yanafuatiliwa na *ZSTC* haihusiki na suala hilo kabisa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, sisi ni wawakilishi wa wananchi na hatuwezi kuleta taarifa ya kubahatisha, kwa sababu itabidi tuombe radhi hilo tunalijua. Mimi ninachotaka kusema ni kwamba haina maana kuwa akishapita kiongozi wa ngazi ya juu tena wengine wote watafuata vile alivyoelekeza, vyenginevyo kusingelikuwa na mahakama, hukumu wala chochote.

Kuna watu wanapewa maelekezo lakini wanatumia fursa kwa kufanya wanavyotaka wao wenyewe. Lakini Mhe. Waziri kaeleza vizuri, wananchi wamesikia na sisi tutazidi kufuatilia na *Inshaallah* tutashirikiana tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nachangia katika kipengele hiki cha 9(1)(e) yaani shirika katika kutekeleza kazi zake chini ya sheria hii litakuwa na uwezo wa kupanga ubora wa karafuu na mazao mengine ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jana nilisema kwamba, ubora wa karafuu unategemea na ukaukaji wa karafuu hiyo au ukaushaji. Serikali imeshindwa kutuletea njia mbadala ya kukaushia karafuu hizi kiasi ambacho siku za mvua zinasababisha kupata mpeta, yaani mpeta ni karafuu zilizokuwa katika *low grade.* Niliwaambia wazi wazi kama ingelikuwa mimi naongoza serikali hii ningeliweza kuleta *special drying plants* ambazo zingekuwa zinakausha karafuu kitaalamu kabisa.

Leo katika kujibu Mhe. Waziri kajibu kijumla jumla tu, kwamba lazima karafuu zitayarishwe kwa muangaza wa jua (*solar energy)*. Mimi ninavyojua *solar energy* sasa hivi inaweza ikafanywa kwa *dynamic energy* na ilikuwa itumiwe kwa shughuli nyengine. Sasa nataka anieleze waziri ni *scientific reason* zipi zinazofanya kwamba karafuu ili iwe ina ubora lazima ipate muangaza wa jua. Sisi tungeweza kuleta *special*

drying grains plants ambazo tutazieneza katika nchi na kuweza kuwapunguzia mzigo wakulima wetu wa kuanika kwa kutumia majamvi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Saleh Nassor mimi sina *scientific research*, lakini nina uzoefu mkubwa hivi sasa ni miaka 30 nafanya biashara najua *what is business, what is marketing and what is demand*, nafahamu kila kitu. Namwambia tena tupatie nchi tatu wewe hizo karafuu nilizokutajia hapa ni nchi gani inakausha karafuu kwa kutumia *scientific method*? Nitajie tu wewe Madagascar, Brazil, Srilanka, Indonesia hamna bwana. *The old method* kukausha karafuu ni jua na utafanya mipango mingine yoyote karafuu unaichakachua, unapunguza *contents* ya *oil*, harufu ya karafuu na kwa hali hiyo karafuu ile inakosa soko.

Hapa si suala la kutaka wewe unataka tu, lakini soko halitaki, mimi mfanyabiashara bwana nitauza biashara kwa mujibu wa soko sio ninavyotaka mimi. Mimi nataka kuzalisha mkoba niutie rangi nyekundu, lakini soko halitaki linataka rangi nyeupe. Kwa hivyo, nikitaka nisitake nitafanya mkoba wenye rangi nyeupe ndio utakaonunuliwa, ukiufanya wa rangi nyekundu utaweka ghalani haununuliwi. Kwa hivyo, mpaka sasa hivi tumeangalia na jana usiku mimi ulinipa kazi mpaka saa tisa naangalia kwenye mtandao kuna teknolojia gani ya kukaushia karafuu.

Mhe. Mjumbe dagaa ipo njia nyengine na tunaifanya iko Ndagoni kaiangalie, lakini sio karafuu, karafuu bado inahitaji kukaushwa kwa jua na hiyo *branding* inayokuja ndio ime-*exist* hasa kwamba karafuu ikaushwe kwa jua. Huo mwani ukaushwe kwa jua tena juu ya uchacha, hayo ni masharti tunayopewa na wanunuzi sio hiari yetu sisi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.*(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu na serikali yetu ina wataalamu sana, kwa kweli wataalamu wetu wanajitahidi sana kutuletea nadharia. Semina za mara kwa mara tunapata kupewa nadharia kadhaa wa kadhaa, lakini nchi yetu inaonekana haiko *dynamic* katika ku-*translate theory into practicals.*

Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kile kipengele cha utafiti katika kuufanyia utafiti mkarafuu sasa iko haja ya Mhe. Waziri na wizara yake kufanya utafiti zaidi katika mkarafuu kuanzia mambo ya upandaji wa mkarafuu, uvunaji na ukaushaji pamoja na uuzaji, serikali wasiwe wavivu. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salim Abdalla Hamad wewe umeshamaliza sasa tunampa Mhe. Rashid Seif Suleiman, wewe umeshamaliza hoja moja tena basi.

Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nikitaka kukumbusha hivyo tu kwamba yeye ameshasema.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nashukuru sana maelezo marefu na mazuri aliyotoa Mhe. Waziri, isipokuwa kwa manufaa ya *hansard* naomba atusaidie. Kwa kuwa alikiri kwamba ushindani aliyoutaja ni ushindani wa soko la nje, nakubaliana naye kwa hapo. Lakini namuomba atusaidie hiki kifungu cha 9(d) kupanga bei ya kununulia karafuu na mazao mengine ya kilimo.

Wakati nilipokuwa nikichangia Mhe. Mwenyekiti, nilitoa rai kwamba, ili maelezo haya yawe na uwiyano basi kuwe na kitu kilichoongezwa kwamba kulingana na soko la dunia. Lakini katika maelezo yake sikusikia kwamba amekitaja kifungu hiki. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi hapa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo kwa kuongeza kipengele, lakini sio soko la dunia *export price*, bei ya kuuzia. Nimetoa semina mimi ya dakika tano hapa kuweka tofauti baina ya **A4B price** na *Marketing price*. Marketing price inajumuisha *logistic*, *duties* na mengineyo. Kwa hivyo, niseme kwamba kutokana na soko la kusafirishia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti kidogo tunatofautiana, pamoja na maelezo yake lakini hiyo *export price* ataitoa wapi *reference* si huko kwenye soko la dunia na kuona kwamba yeye auze vipi kwa yule muuzaji. Sasa anaona tabu nini kuingiza maneno hayo? Hiyo *export price* iingie lakini kulingana na bei ya soko la dunia, sio kwamba auze vile vile bei ya soko la dunia, lakini ilingane na soko la dunia kwa hiyo njia anayoitaka yeye. Tuendelee.

Kifungu cha 9 - Uwezo wa Shirika pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA TATU – UONGOZI WA SHIRIKA

Kifungu cha 10 - Uteuzi wa Mkurugenzi Mwendeshaji pamoja na marekebisho yake

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia na nashukuru Mhe. Waziri alilitaja hili suala, lakini kidogo naomba ufafanuzi. Kwa sababu katika pendekezo tulilotoa mimi nilitoa pendekezo kwamba itofautiane baina ya Bodi ya Wakurugenzi na huyu Mkurugenzi Mwendeshaji katika utawala wake. Alikubali kwamba iwe tofauti kuwa asichaguliwe kwa kipindi kwa kipindi, lakini naona katika maelezo yake alitaja miaka kumi. Sasa sikumfahamu kwamba itakuwa baada ya miaka mitano sasa itakuwa kumi.

Kwa sababu mimi katika mchango wangu ilikuwa ni kama muajiriwa asiwe na kikomo, aendelee na kazi yake kama muajiriwa mwengine atakapofanya makosa tena mambo mengine, lakini isiwe kama miaka kumi au tisa au mingapi. Hebu atupe ufafanuzi kidogo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika maelezo yangu nafikiri hawakunifahamu tu wajumbe, mimi nimekubaliana nao moja kwa moja kwamba huyo mtendaji atakayeteuliwa na rais ataendelea kwa muda wote mpaka afe au ajiuzulu, *provide* ametimiza masharti. Kwa sababu kwa mujibu wa katiba hii rais anayo mamlaka ya kumtoa madarakani mtu yeyote aliyemuweka, kumpandisha cheo, kumhamisha, kumuongezea madaraka au kumpunguzia. Kwenye kifungu cha 53(b) rais ana mamlaka kwa hivyo mimi sina matatizo yoyote ni muwafaka na akae tu mpaka achoke.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namuomba radhi kama sikumfahamu vizuri, pili naomba tuendelee.

Kifungu cha 10 - Uteuzi wa Mkurugenzi Mwendeshaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 11 - Uteuzi wa Maofisa wa juu pamoja na maofisa wengine pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 12 - Uteuzi wa wakala na wakandarasi
Kifungu cha 13 - Bodi ya Wakurugenzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 14 - Katibu wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 15 - Uwezo wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 16 - Bodi kuwa na mamlaka ya kinidhamu
Kifungu cha 17 - Mkutano wa Bodi na Serikali pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA NNE – MASHARTI YA FEDHA

Kifungu cha 18 - Fedha na mali za shirika
Kifungu cha 19 - Matumizi na bajeti pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 20 - Hesabu na ukaguzi

SEHEMU YA TANO – MASHARTI YA JUMLA

Kifungu cha 21 - Miongozo ya waziri pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 22 - Makosa na adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 23 - Kosa kwa taasisi inayojitegemea
Kifungu cha 24 - Kosa kwa kutumia wakala
Kifungu cha 25 - Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 26 - Mazao mengine ya kilimo
Kifungu cha 27 - Uwezo wa kufanya sheria ndogo ndogo pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 28 - Kufuta na kubakiza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na masahihisho yake sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji waliokubaliana na Mswada wa Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Shirika la Taifa la Biashara ya mwaka 2011

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Shirika la Taifa la Biashara ya Mwaka 2011 usomwe kwa mara ya pili.
Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji waliokubali Mswada wa Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mswada wa Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa la Biashara sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa kazi kubwa tuliyofanya na tumshukuru Mhe. Waziri tumpongeze kwamba mswada wake umepita. Kwa hivyo, kwa kuwa kazi tuliyoifanya tumeimaliza na hatuna nyengine naomba kuahirisha kikao chetu hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 19/10/2011 saa tatu za asubuhi.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 19/10/2011 saa 3:00 asubuhi)